CHUO CHA BIBLIA

NDOA NA JAMII
(Sehemu Ya Pili)

KITABU CHA SABA

Viunganishi Saba Vya Umoja

Hiki ni kitabu cha pili cha nakala ambazo zinakukumbusha kuhusu yale ulioyasikia katika vipindi vyetu vya redio kuhusu ndoa na jamii. Ikiwa hauna nakala ya kwanza, jaribu kukipata na kukisoma kabla ya kusoma nakala hii. Kwa hakika, utapendezwa zaidi na kitabu hiki baada ya kusoma kilichotangulia katika hoja hii.

Hili kuelewa vipindi vyetu redio ni pamoja na vijitabu hivi viwili, ni lazima ufahamu kuhusu mfano ambao ulihusika katika mfumo wa masomo haya yote. Hivyo basi, inanibidi kurudia maelezo yangu kuhusu mfano ambao uko katika kitabu kilichotangulia. Baada ya mfano huu kuelezwa kwa mara ya pili, nitaendelea kutoka mahali pale ambapo kijitabu cha kwanza kulimalizikia.

Mwaminifu mmoja wa asili ya Afrika aliuchonga mfano wa kuvutia sana wenye maelezo mazuri kuhusu kusudi la Mungu wakati alipowaumba wenzi wawili wa kwanza na kuwatangaza kuwa ‘mwili mmoja.’ Wakati mwaminifu huyu mwenye usanifu mkuu alipochonga sanamu hii, alikuwa akidhihirisha kwa mfano njia saba ambazo mume na mke wanahitajika kuwa ‘mwili mmoja.’

Sanamu hii ya mume na mke. Wao wameunganishwa pamoja kwa kiunganishi cha minyororo miwili-miwili saba. Kiunganishi hiki ambacho kinawaleta pamoja kila mmoja juu ya kichwa chake. Kila moja ya viunganishi hivi kinawakilisha maeneo kuhusu umoja ule Mungu aliokusudia. Viunganishi vilivyo juu ya vichwa vyao vinawakilisha uhusiano alionao kila moja wa kiroho kwa Mungu. Kweli kwamba viunganishi vingine vimeunganishwa kwa viunganishi vilivyo vichwani mwao ni dhihirisho kwamba uhusiano wao wa kiroho ndio msingi wa maeneo mengine yote katika umoja wao.

Viunganishi viwili vya kwanza vinawakilisha mawasiliano ambayo ni chombo kinachowawezesha kuweka na kudumisha umoja wao. Kiunganishi kinachofuata ni utangamano ambao ni ishara ya umoja wao. Katikati mwa viunganishi hivi vitano, vinawakilisha upendo, ambao ndio uwezo au nguvu za umoja wao. Kiunganishi cha upendo kinafuatiwa na cha

ufahamu, ambacho kinawakilisha kukua katika umoja. Viunganishi vya mwisho ambavyo vinawafanya kuwa mwili mmoja ni ngono au kujamiiana, ambavyo ni dhihirisho lenye furaha kuhusu umoja wao.

Dhihirisho kwamba viunganishi hivi ni viwili. Inaonyesha kweli kwamba maeneo haya yote ya umoja ni ya kubadilishana au kutendeana mmoja kwa mwingine, au vinahusika katika kupeana na kupokea kati ya mume na mke. Unapounganisha viunganishi vitano kwenye viunganishi vilivyo juu ya vichwa vyao ambavyo vinawakilisha uhusiano wao wa kiroho ambao ni lazima kila mmoja kuwa nao kwa Mungu, utapata viunganishi saba vya umoja.

Vipindi vya redio kuhusu ndoa na jamii vilitokana na hatua hizi saba za ndoa ambayo iliwakilishwa na viunganishi saba vinavyomfanya mwanamume na mkewe kuwa mwili mmoja. Katika vijitabu hivi viwili, ningelitaka kukupa muhtasari wa yale uliyoyasikia toka kwenye kipindi cha redio kuhusu sheria ya Mungu katika ndoa na jamii.

SURA YA KWANZA

Kiunganishi Cha Ufahamu

Katika mashauri na wenzi walio katika ndoa, bila shaka unasikia lalamiko moja mara kwa mara: 'Yeye hanifahamu mimi.' Au, 'Yule hanielewi mimi.' Kutofahamiana kati ya wenzi hao ndio sababu iliwafanya kujadili kuhusu ndoa yao na washauri au mchungaji. Maelezo yetu ya ufahamu ni, 'makubaliano au mapatano yanayotatua tofauti.' Maelezo mengine ni, 'utambuzi wa dhana au mawazo na makusudio yanayoleta ufahamivu na ushirika katika maono ya watu wawili.'

Mtume Petro anawashauri waume kuishi na wake zao kwa akili; na kumpa heshima **(1 Petro 3:7).** Mume, je! unamfahamu vipi mkeo? Ikiwa yeye angehusika katika ajali ya gari na madaktari wakuite kwenye hospitali, na kuuliza ikiwa unaweza kuwapa historia yake yote ya kiafya, je, unaweza kufanya hivyo? Ikiwa angefanyika mwenda wazimu, ungeweza kutoa historia yake yote kuhusu ushirika na uhusiano wake wote wa kiafya? Pia ni muhimu kuwauliza wake maswali haya. Je! Wewe unamfahamu kiasi gani mumeo? Je! Mnafahamiana vipi mmoja kwa mwingine? Na je! Mnafahamiana na kuelewana?

Je! Umuhimu wa ufahamu ni upi katika ndoa? Umuhimu wake ni upi kwa umoja kati ya mume na mke? Sidhani kwamba tunaweza kutilia mkazo zaidi kuhusu umuhimu wake ikiwa watu ambao wameunganishwa pamoja na Mungu wanahitajika kuwa na ushuhuda wa yale Mungu aliyowaandalia katika kupata ujuzi wa ndoa yao. Ikiwa washiriki wote wawili wa ndoa binafsi au kwa pamoja, wana uhusiano pamoja na Mungu, na ikiwa katika uhusiano wa mmoja kwa mwingine wanadhihirisha kwa furaha mawasiliano, utangamano, upendo na ufahamu, hivyo basi, viunganishi hivi vya umoja vitaonyesha tofauti kati ya uhusiano wa jinsi ya kuishi pamoja, na uhusiano wa ndoa ya kweli ambayo Mungu alitayarisha wakati alipomfanya mwanamume na mwanamke kuwa mwili mmoja.

Nimekuwa na ujuzi wa miaka mingi katika kuwafikia watu kwa njia ya uinjilisti hasa waume ambao walikuwa na mawazo asili kwa wake zao. Na nyakati nyingi, nimewaambia hivi: 'Tilia maanani kila kitu ambacho mkeo anakutendea. Kama ungekuwa tajiri, ungenunua vitu vyote. Ungenunua hata ngono. Hata ungemchukuwa mke wa makamu akuzalie watoto na hata kuwalea na kuwa mlezi wao. Lakini kuna kitu kimoja ambacho hauwezi kununua, ambacho ni uhusiano ambao Mungu alifanya kwa mwanamume na mkewe.

Kama watu wa kiroho, tunaotafuta mwongozo wa kiroho na wa kibiblia katika ndoa na jamii, tunahitajika kuanza kwa kukiri kweli kwamba Mungu ndiye aliyefanya ndoa kuwa uhusiano au ushirika. Tunapojenga uhusiano huu pamoja, kuelewana ni sharti kuwe jiwe la msingi katika ujenzi wetu. Mawasiliano yetu ndio chombo cha kupalilia na kudumisha umoja. Utangamano ni dhihirisho la umoja. Upendo wa utukufu ndio uwezo au nguvu zinazoendesha umoja wetu, ilhali

kufahamiana kutazalisha kukua kwa umoja wetu. Ikiwa tutafahamiana, tunaweza kujenga na kuona uhusiano wetu ukikua.

Miaka mingi iliyopita, daktari mmoja Mswisi mtaalamu wa magonjwa ya ki-akili aliyekuwa mwaminifu, aliandika kitabu kizuri sana kinachoitwa, 'Kumfahamu kila Moja.' Katika sura za kitabu hiki, Daktari *Paul Tounier* anatuambia kwamba kumfahamu yule mwingine, ni lazima tuwe na nia ya kumfahamu mwenzio; ni lazima tuwe na ujasiri wa kuwasiliana vyema; na ni lazima kuwepo na maeneo ya kiroho katika ndoa yetu.

Hebu wazia juu ya hatari za kutofahamiana. Katika sehemu nyingi ulimwenguni, kuna janga kuu na tauni katika talaka. Katika desturi au mila nyingi za ndoa, mume humwacha mkewe na kuelekea kazini, ilhali mke ana wajibu wake nyumbani na watoto. Mume huku akiwa amevalia nadhifu na kuvutia akiwa kazini hufanya kazi na wanawake ambao pia huwa wamejivika nadhifu na kuvutia. Kwa wakati mwingine, mwanamume huyu katika mazingira haya huwa na mawasiliano mengi na katibu wake zaidi ya mkeo. Yeye humfahamu vyema, na kuzungumza naye kwa wakati mrefu. Hivyo basi, si jambo la ajabu kwamba huyu katibu wake, au mwanamke mwingine yule ambaye hufanya kazi pamoja naye, huanza kuichukua nafasi ya kwanza katika maisha, na ndoa yake kuvunjika katika talaka.

Pia kuna mamilioni ya ndoa ambazo wote wawili, huondoka nyumbani na kuelekea kazini kila asubuhi. Ikiwa hawa wawili katika ndoa ni wenye kujimudu katika kazi, kiasi kwamba hawana fursa ye yote katika uhusiano wao na hawafahamiani, ni kwa muda kidogo tu mtu mwingine afanye hivyo. Kwa kuwa watu wana haja kuu ya kufahamika, yule mume - au mke - siku moja atakutana na mtu ambaye anamjali kiasi kwamba atamfahamu.

Mtu mmoja aliokoka baada ya muda mrefu katika dhambi na upotovu mkuu. Mchungaji mmoja alikuwa akikutana naye mara tatu kila juma kwa muda wa miaka mitatu hili kumfanya mwanafunzi mwema wa Kristo. Alivyozidi kumfahamu, alijifunza baadhi ya mambo kutoka kwake. Kabla yake kumjia Kristo, alikuwa na sifa za kuzini pamoja na wake wa watu ila mkewe. Yeye alikuwa mkubwa na mzuri wa uso, mwenye uzungumzi mpole. Alisema kwamba wakati mwingi, wanawake ndio waliokuwa wakimfuata kwa bidii. Yeye alitambua hivi: '*Wanawake wale niliokuwa na uhusiano nao hawakuwa na haja ya mpenzi. Hawakuwa wakifatuta mtu wa kufanya mapenzi naye bali walikuwa na haja ya mtu wa kuzungumza nao. Wao waliniambia kwamba waume zao hawakuwa na wakati wa kuzungumza nao, na hawakuwafahamu. Hivyo basi, walizungumza nami hata kuamini kwamba mimi niliwafahamu.*'

Hapa tunasikia kinyume cha hadithi hii. Mume ambaye mke wake hamfahamu huwa katika hatari ya kutumbukia kwenye uhusiano mwingine. Ni hatari kupuuzia haja ya mwenzio la kufahamiana. Katika michezo mingi, kinga njema ni ule uvamizi wenye nguvu. Kinga iliyo bora dhidi wa wenzi wetu hutokana na mtu mwengine kutenda kazi kwa kukuza ule umoja wetu kama wenzi. Umuhimu wa hali hii ya ukuaji hutokana na sisi wenyewe kutenda yale yote tuwezayo katika kuwafahamu wenzetu.

Kusheherekea Tofauti

Hapa ni mahali pema pa kuanza kumfahamu mwenzio: Kuna tofauti kati ya mume na mke. Kuna tofauti za kimwili, biolojia, mawazo, hisia na hata hali ya kiroho kati yake mwanamume na mwanamke. Kuna tofauti kati ya jinsi mume na mke wanavyofikiria, kutenda mambo, kuhisi mambo na hata kukumbana na mazingira yake. Wanaume na wanawake pia huabudu Mungu kwa njia moja.

Jambo hili lilidhihirika kwa mchungaji mmoja miaka mingi iliyopita kwa njia ambayo ni vigumu kusahau. Mke wa daktari mmoja alimtembelea. Alikuwa mtu wa kuvutia kwa umbo, mcha Mungu aliyejitolea kabisa Kwake, alikuwa amejitolea kabisa katika huduma Kanisani mwao kwa kuongoza maombi, pamoja na mambo mengine. Mchungaji huyo alikutana naye katika mazingira ya huduma Kanisani. Mume alikuwa daktari wa upasuaji maarufu sana lakini huku machozi yakimtiririka usoni mwake, alisema haya, 'Mimi nina mzigo mkuu kuhusu mume wangu. *Yeye kwa*

hakika si mtu wa kiroho; si wa kiroho kamwe.' Mhudumu wa Mungu alimjibu, 'Naam, tunahitajika kuliombea jambo hilo, kwa kuwa ni Mungu peke yake awezaye kumfanya kuwa mtu wa Kiroho.'

Miezi mitatu baadaye, mchungaji huyo aliitwa kuhudumu katika tahadhari ya mwanamke mshiriki wa Kanisa lao aliyekuwa mgonjwa mahututi ambaye alikuwa na shida ya nyongo na moyo. Nyongo yake ilihitaji kutolewa, lakini ilikuwa hali ya tadhari kwa kuwa moyo wake ulikuwa dhaifu. Mchungaji huyo alikuwa hospitalini pamoja na mumewe huyu mgonjwa, wakinzungumza kando wakati 'daktari asiye wa kiroho' alipomwita mchungaji nje ya chumba kile. Alimwambia hivi, *'ninahitaji kutoa hii nyongo, isipokuwa kuna hatari kuu. Hospitali ina chumba kidogo cha maombezi huko chini. Je! Unaweza kwenda huko chini na kuomba hadi wakati nitakapomtuma mwuguzi kukuambia kwamba tumeepuka hatari kuu?' Naye akamjibu, 'naam niko tayari. Nitakwenda kwenye chumba kile na kufanya maombi kwa niaba ya yule mama mgonjwa.'*

Mchungaji huyo alielekea kule chini katika chumba cha maombi na kuomba. Ilipotimia saa tano asubuhi, alikuwa na ushuhuda wa kiroho katika maombezi kwa yule mke, kiasi kwamba alifahamu kuwa Mungu alikuwa ametenda jambo fulani. Baada ya dakika kumi na tano, mwuguzi alikuja katika mlango wa chumba kile cha maombezi na kusema, *'Daktari anasema kwamba mambo yote ni shwari. Tumepita tayari pale palipokuwa na hatari kuu.'*

Baada ya upasuaji huo, kabla ya yule daktari kusema neno moja kwa mume wa yule mgonjwa, alimwendea mchungaji huyo kwa haraka sana na kutikiza mikono yake na kusema, 'Ahsante sana kwa maombezi yako. *Ahsante sana. Ilikuwa ni miujiza kwetu kupitia hali hiyo.'*

Huyu ndiye yule daktari ambaye mkewe alimtaja kuwa asiye mtu wa kiroho. Wakati walipokutana tena, alimwambia yule mwanamke, 'Nadhani kwamba wewe ulikosea kabisa katika yote. Mume wako ni mtu wa kiroho mno.' Yule mwanamke alilia wakati alipoelezwa yale aliyokuwa ametenda. Huyu daktari alikuwa mtu wa kiroho, walakini, hakudhihirisha hali hiyo kwa njia ambayo mkewe aliyodhihirisha yake. Hivyo basi, yule mke alidhani kwamba mumewe hakuwa wa kiroho maishani mwake. Hii pia ilionyesha kwamba kwa hakika yeye hakumfahamu mumewe vyema.

Ikiwa tutawafahamu wenzi tunaoishi nao, ni lazima tutambue na kufahamu tofauti zilizopo kati ya wanaume na wanawake. Uume na uke ni maumbile yaliofanywa kuwa tofauti. Tofauti hizo ndizo zilizokuvutia kwa mwenzio na kumfanya kuvutiwa nawe. Mke huvutiwa na mume kwa sababu ya ajali ya uume wake. Naye mume huvutiwa na mke kwa ajili ya uke wake. Tofauti hizi zinahitajika kusherehekewa wala sio kutatuliwa. Ni jambo la kufedhehesha kwa mwanamke kuambiwa kwamba hili aheshimike, ni lazima kuiga tabia na jukumu za mume. Hili silo linalomwezesha mwanamke kuwa na heshima yake. Kwa hakika kinyume chake ndio kweli. Jukumu na wajibu wa mke ndio humpa heshima yake. Pia ni kweli kwa upande ule mwingine. Waume watapata heshima na stahi yao katika kutimiza jukumu na wajibu uliokusudiwa na Mungu kwao waume.

Ikiwa wawili wetu wangekuwa wamefanana kabisa, ni kweli kwamba mmoja hangehitajika. Mungu ametuumba tukiwa tofauti kwa sababu, kama vile tulivyojifunza katika nakala ya uumbaji ya kitabu cha Mwanzo, tofauti zetu hutosheleza na kutimizwa hadi tunapofanyika kuwa mtu mmoja mkamilifu 'Adamu.' (Mungu akawaita jina lao kuwa 'Adamu,' wala sio 'bwana na bibi Adamu' **(Mwanzo 5:1).** Mpango wa Mungu ulikuwa na bado ni - sio aidha/au, bali ni wote wawili/na wakati Mungu anapoumba mume na mke kuwa mwili mmoja.

Umuhimu Wa Yaliyopita

Sote tunaumbwa na matokeo ya ushuhuda wetu katika maisha. Kwa miaka yote ambayo mlipata kuishi kabla ya kukutana, mlikuwa mkiumbika na kufanyika jinsi mlivyo ki mazingira na jamaa zenu walivyo washawishi kuwa watu mliokuwa kabla ya kukutana. Ikiwa mtapata kufahamiana mmoja kwa mwingine, ni lazima ufahamu umuhimu wa ushawishi wa yale yaliyopita ambao uliwafanya jinsi mlivyo leo. Hebu tazama mfano huu:

Katika miaka ya sitini, mke wa mchungaji mwandishi wa kitabu hiki kwa jina *Ginny* alikuwa mgonjwa sana. Kwa hakika, watu waliowafahamu wakati ule ambao kwa sasa wanawatembelea, wangetarajia kumpata katika kiti cha magurudumu. Mchungaji huyo alipofika nyumbani siku moja, *Ginny* alikuwa na homa kuu pamoja kuvimba katika viungo vyake vyote. Alikasirika na kuhadhirika sana. Kwa hakika, alipiga teke kitanda chake! Kwa kweli hili si jambo ambalo mkewe alitarajia kutoka kwa mumewe. Kwa aibu kuu mchungaji huyo hakuwa mfano mwema wa mume! Lakini hapo baadaye, lilikuwa jambo la muhimu kwao kurudi nyuma kwa yale yaliyopita na kuona kana kwamba wangefahamu sababu ya kukambiliana na ugonjwa kwa njia hiyo.

Mchungaji huyo, alipokuwa bado mchanga, mamake alikuwa mgonjwa sana. Walikuwa watoto kumi na mmoja katika nyumba ile, sio muda mwingi baada ya kitinda mimba kuzaliwa, mamao alipopatikana kuwa na ugonjwa wa saratani ya sehemu ya chini ya tumbo *(Colon Cancer)*. Baada ya upasuaji mkuu na miaka miwili zaidi ya ugonjwa, Mungu alimchukua. Wakati huo, mchungaji huyo alikuwa akimtazama babake. Alikuwa na nyumba yenye watoto wengi pamoja na mke aliyekuwa mgonjwa. Yeye alikuwa mchana kutwa akisambaza barua na usiku akiendesha gari la kupanga *(Taxi)* ili kukidhi jamii yake pamoja.

Wazo lilikuwa likichimbuka ndani ya mchungaji huyo: 'Wanawake huwa wagonjwa na kukuachia nyumba iliyojaa watoto.' Wakati mkewe Ginny alipopatwa na ugonjwa, walikuwa na wana watano, wawili kati yao walikuwa bado wakitambaa ilhali watatu walikuwa bado wachanga. Basi alipoingia nyumbani siku ile na kumpata katika maumivu, ushawishi wa masaa yote aliyomtazama mamake akifa huku babake akisumbuka ulimfanya kukambiliana na janga hilo kwa njia ile. Walipochambua hayo yote, haikuwa vigumu kwao kuelewa ni kwa sababu gani alikuwa na hasira na dhiki wakati mkewe alipokuwa mgonjwa.

Lilikuwa jambo la muhimu kwa mkewe *Ginny* kufahamu alipozoa ushuhuda wake uliopita. Ikiwa hangefanya hivyo, basi labda angetafuta cheti cha talaka! Lakini badala yake, alichukua fursa ya kufahamu chanzo cha hasira na dhiki yake. Mwishowe, ilimbidi mchungaji huyo kujisemea mwenyewe, 'kuwa na moyo mwanamume! Huyu si mamako. Huyu ni mkeo, na anahitaji usaidizi wako.' Kuna nyakati nyingi anasaidika kwa kufahamu yale yanayomshawishi na kumfanya mkewe kuwa jinsi alivyo leo. Ikiwa unahitaji kumfahamu mtu ambaye unaishi naye, ni lazima utambue umuhimu wa yale aliyoyapitia.

Utakatifu Wa Ubinafsi

Mungu alikusudia kila mmoja wetu kuwa wa kipekee au maalumu. Yeye hutupilia mbali mfano wakati wote anapoumba mmoja wetu. Neno 'nafsi' limeelezewa katika kamusi kama *'Upekee, ubinafsi wa mtu ye yote unaomfanya kutambulika kutokana na mtu mwingine.'* Nimetambua kwa muda mrefu kama mchungaji kwamba, mmojawapo ya msingi wa maelezo kuhusu kutokuwa na furaha ni kwamba watu sio Nani, Kipi, na Wapi Mungu amewapangia kuwepo. Mume na mke wanaweza kusaidiana kugundua mahali utu ambao Mungu amewapa uko pamoja na mapenzi mema, ya kupendeza na kamilifu ya Mungu katika maisha yao **(Warumi 12:1,2).**

Hili ni hoja kuu wakati tunapotilia maanani umuhimu wa kufahamiana katika ndoa. Mtu fulani alifafanua ufahamu kama 'makubaliano ambayo husuluhisha tofauti.' Je! Hii si ni fafanuzi ya kuvutia sana kuhusu ufahamu? Fafanuzi nyingine inasema hivi, 'makubaliano ya dhana na nia ambayo huleta utambulizi na ushirika katika maono ya wengine.' kwa kumfahamu mtu ambaye unaishi naye, inakubidi kufahamu tofauti kati ya mume na mke. Pia unahitajika kufahamu umuhimu wa yale yaliyopita.

Kumwelewa mwenzio, ni lazima ukusudie na kutaka kumfahamu. Watu wengine katika ndoa hawataki kutumia wakati wao pamoja na uwezo wa kihisia ambao unahitajika kumfahamu mwenzio. Je, na wewe? Je! Kweli unataka kumfahamu mwenzio? Ikiwa unahitaji kufanya hivyo, yafuatayo ni baadhi ya mashauri.

Kwanza, kuelewa mwenzio, ni lazima kutimiza matakwa ya Amri Kuu. Yesu alisema, *'basi, yo yote, myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii'* **(Mathayo 7:12).** Hii ndio aya kuu katika Biblia kuhusu uhusiano wa wanadamu. Ili kutimiza mafundisho haya, wanawake ni lazima wajiulize, *'Kama ningekuwa mume wangu, ni jambo gani ambalo ningetaka mke wangu kunitendea?'* Nao waume wanahitajika kujiuliza, *'Ikiwa ningekuwa mke wangu, ni jambo gani ningemtaka mume wangu kunitenda?'* Hii ni kinyume na asili ya kibinadamu ya ubinafsi ya kujitakia wenyewe, lakini ikiwa tutamwuliza Mungu kutupa neema, tutaweza kuwa wenye kuwatakia wenzio na kujumuisha Amri Kuu ya Yesu huku tunapozidi kufahamiana.

Pili, lazima tuwasikilize wenzetu. Usikivu kwa hakika ni hali ya usanifu, na kuna mengi ya kujifunza kuhusu kusikiza ambayo wengi wetu bado hatujajifunza. Wakati mwingine ni dhahiri kwamba mume na mke hawasikilizani. Wakati wanaposema kwamba wanawasikiliza, yale ambayo wanamaanisha ni kwamba, *'Mimi ninafikiria nitakalokuambia wakati utakapofunga kinywa chako!*' Yesu alisema, 'mwenye masikio, na asikie' **(Mathayo 11:15).** Je! Wewe unamsikiza mke au mume wako wakati anapojaribu kuwasiliana nawe?

Injili ya Luka inanakili hadithi moja inayomwelezea Yesu akimtembelea Farisayo mmoja nyumbani kwake. Mwanamke anaingia ndani na kulia wakati anapogundua kwamba yule Farisayo hakuwa ameitawadha miguu ya Yesu. Hii ilimaanisha kwamba yule Farisayo alikuwa hajampa makaribisho kamili Yesu. Aliachilia machozi yake kumwagika juu ya miguu ya Yesu, kisha kuipangusa kwa nywele zake. Naye Farisayo yule anawaza, 'kama angelimjua huyu mwanamke jinsi alivyo, asingemruhusu kutenda yale.

Lakini wakati Farisayo anapokuwa akiwaza hayo, Yesu anamwuliza swali muhimu. *'Simoni, Je! Unamwona mwanamke huyu?'* Kuna maneno ya aina nyingi katika lugha ya Kiyunani kuhusu neno 'kuona.' Katika tukio hili, neno ambalo Yesu alitumia linamaanisha, 'Kwa hakika wewe unamwona huyu?' au, 'ni jambo lipi unaloliona wakati unapomwona mwanamke huyu? Nadhani hili ni swali nzuri sana kwa waume. Je! Kweli wewe unamwona yule mwanamke uliyemwoa? Je! Wewe unamsikiliza mke wako wakati anapojaribu kuwasiliana nawe?'

Francis wa Assisi ni mmoja wa watu wanao vutia sana. Yeye alipojiunga na chuo cha seminari, ilikuwa ni habari kuu kwa kuwa alikuwa kutoka jamii kuu. Baada ya kumaliza masomo yake katika seminari (ambayo siku zile iliwalazimu kutembea kote wakiwa na vikapu shingoni mwao kwa miaka kadhaa huku wakiomba chakula kuthibitisha kwamba wametupilia mbali ulimwengu, mwili na shetani), wakati wa kufanywa kasisi *(ordination),* ilikuwa desturi kwamba yule anayefanywa kasisi ni lazima ahubiri. Kanisa lilijaa siku ya Francis kufanywa kasisi kwa kuwa alikuwa mtu aliyejulikana sana kabla ya kujiunga na watawa. Aliposimama kuhubiri, kila aliyehudhuria alifikiri kwamba hayo ndiyo mahubiri makuu yaliyowahi kuhubiriwa. *Alisema, 'Mungu hakuniita kuhubiri ila kutenda. Hebu na tuombe.'* Naye akafanya maombi haya:

'Bwana, nifanye chombo cha amani yako. Pale pana chuki, nanipande upendo; pale pana majeraha, rehema; pale pana shaka, imani; pale pana tamaa, tumaini; pale pana giza, nuru; na palipo na huzuni, furaha. Ee, Mungu mkuu, nisaidie hivi kwamba nisitarajie kufarijiwa bali kufarijiana; nisifahamike bali nifahamu; kupendwa ila nipende. Kwa maana ni katika kutoa tunapokea; katika kuhurumia, tunahurumiwa, na katika kufa ndipo nasi tunapozaliwa kwenye uzima wa milele.'

Hayo ni maombi mwafaka yenye wazo la ajabu ambalo tunapaswa kuiga katika changa moto ya kuwafahamu wenzetu katika ndoa. *'Niwezeshe nisipate kufahamika bali nifahamu.'* Msingi wa kumfahamu mwenzio unayeishi pamoja naye ni kumjali na kumweka mbele ya mambo mengine. Hili kumfahamu mwenzio, ni lazima 'kusoma kwa makini' na 'kusikia vema sana' haja za mwenzio.

Sawa na mafunzo ya Yesu, sala hili la *Francis* linatupatia dhana nyepesi mno. Lakini kweli hii nyepesi linaweza kuwa na mageuzi makuu wakati inapohuzishwa katika ndoa yako. Ukweli ni kwamba, mfanye mwenzio awe kina cha katikati wala usihofie kufahamika. Jambo

ambalo unastahili kuhusika nalo zaidi sio kwamba mwenzio akufahamu, bali wewe kumfahamu. Hoja sio unapokea upendo, bali unapeana mwenyewe.

Undani Wa Mawasiliano

Ili kumfahamu mwenzio, ni lazima uwasiliane naye katika kiwango cha undani. Kuna viwango tofauti vya mawasiliano katika ndoa. Kwanza, kuna kiwango cha kutokuwasiliana, kiwango cha juu ambapo wewe na mwenzio hamzungumzii mambo ya muhimu. Kwa kiwango, mnazungumzia kuhusu yale mnayofahamu. Kwa undani zaidi, mnazungumzia kuhusu yale mnayofikiria na jinsi mnavyohisi. Na kwa undani kabisa, huanza kuzungumzia kuhusu nani, nini na wapi mlipo katika maisha yenu jinsi inavyohusu Mungu anataka uwepo.

Hii ni zaidi ya mazungumzo machache ya kawaida kama 'nipatie hiyo chumvi' au 'leo mvua itanyesha.' Unapowasiliana katika kiwango cha mapana marefu, huwa umeiweka roho yako katika mikono ya mwenzio, na anaweza kufanyia lo lote hiyo roho yako. Anaweza kuitupa chini na hata kuikanyanga. Na labda lililo mbaya zaidi, anaweza kuipuuzilia mbali.

Jambo lililo mbaya zaidi nililowahi kusikia kutoka kwa mtu kuhusu mwenziwe lilikuwa wakati wa ushauri. Huyu mtu alikuwa mkubwa mwenye uso wa ukatili. Mkewe alikuwa kwa muda wote akimwuliza, *'unafikiria nini kunihusu? Wewe unanifikiria vipi?' Mwishowe, alimtazama mkewe na kumwambia, 'Wewe mwanamke, unajihadaa mwenyewe.* Mimi sifikirii juu yako hata kidogo.' Kinyume cha upendo sio chuki; ni kupuzia. Huyu mume alikuwa akiwasiliana kinyume cha upendo wakati aliponena maneno hayo kwa mkewe.

Ukiweka moyo wako kwenye mikono ya mwenzio, unaweza kuumizwa. Lakini hautaweza kufikia kiwango cha kufahamu hadi wakati utakapokusudia kujitolea bila vikwazo vyo vyote. Kuwasiliana katika kina kirefu, humaanisha kufahamu kukabiliana na shida. Unapoingia kwa undnai katika mawasiliano, mwenzio atasema yale ambayo hutaki kusikia. Hii ndiyo sababu Daktari Tounier aliandika sura kuhusu 'Ujasiri Wa Kuwasiliana.' Wakati mwenzio anaposema kitu ambacho unahitaji, lakini hutaki kusikia, unaweza kujitenga au unaweza kujifunza jinsi ya kukumbana na pingamizi zitokazo katika kina kirefu cha mawasiliano.

Kukabiliana Na Hasira

Wenzi wanaowasiliana katika kina kirefu wanahitajika kujifunza jinsi ya kukabiliana na hasira. Watu tunao wapenda sana wana uwezo wa kutukasirisha sana Hasira ni hisia ya kustajabisha sana. Je! Unafikiria vipi juu ya mwamini mwenye hasira katika maisha yake? Je! Unafikiria kwamba Mungu anataka mwamini mwenye kujawa na Roho Mtakatifu kuwa na hasira? Je! Hasira ni hisia inayokubalika kwa mwanafunzi wa Yesu? Sikiliza maneno haya ya Paulo kuhusu hasira katika maisha ya waumini:

'Muwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe Ibilisi nafasi..... Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya' **(Waefeso 4:26, 27, 30, 31).** Yakobo anatupatia ushauri wa wazi kuhusu hasira wakati anapoandika: *'Kwa maana hasira yake mwanadamu haitendi haki ya Mungu'* **(Yakobo 1:20).**

Mtazamo Wa Kibinafsi

Nilikuwa mwaminifu lakini mwenye hasira nyingi nilipofunga ndoa. Nilijiambia hiyo ilikuwa ni hasira takatifu, lakini ilikuwa wazi kwamba haikuwa hivyo hata kidogo. Ilinibidi kutafuta Maandiko kuhusu yale Mungu aliyoyanena kuhusu hasira. Wakati mmoja, nilipiga konde redio yangu, na kuitomboa tundu kubwa juu yake. Ilionekana kana kwamba bomu ilikuwa imeipiga! Tulipohama baada ya miaka kadhaa, *Ginny* mke wangu alikuja na ile redio pale tulipohamia. Aliiweka kando ya kitanda changu kwenye meza dogo la kuwekea vitabu ili niweze kukumbuka.

Mimi nilijaribu kumweleza kwamba kwa hakika, sikuwa na hasira dhidi yake. Nilifadhaishwa na afisa mmoja wa benki nilipokuwa nikitafuta mkopo. Nilikuwa na hasira ya matumizi mabaya wa fedha zetu, hivyo basi nikaipiga redio yetu.

Kuna maswali ambayo unahitaji kujiuliza kuhusu hasira. Mbona umekasirika? Umekasirishwa na nani? Chanzo cha hasira yako ni nini? Kwa wakati mwingi, chanzo cha hasira yako huwa wazi sana kwa yule tunaye mwelekezea. Wakati mwingi huwa tumejikasirikia wenyewe, jinsi nilivyokuwa. Labda wewe umekasirishwa na tajiri wako na huwezi kumpiga. Kwa hivyo, unapofika nyumbani, unavunja vitu. Ingawa inaonekana kana kwamba wewe una hasira kwa mwenzio, naye pia anafikiria kwamba unamwelekezea hasira inawezekana kwamba hauna hasira kinyume cha mwenzio. Hata inawezekana kwamba hauna hasira kinyume cha tajiri wako. Labda una hasira na nafsi yako. Ni jambo la muhimu ikiwa wewe pamoja na mwenzako mnaweza kufahamu ni nini kiini cha hasira yako.

Ni dhahiri katika kifungu kuhusu hasira tulichosoma hapo awali kwamba Mungu hataki mwamini mwenye kuongozwa na Roho Mtakatifu kuwa na hasira. Katika Agano Jipya tunasoma haya: *'Uwe na hasira lakini usitende dhambi'* **(Waefeso 4:26).** Watu wengi hufanya maneno hayo matatu ya kwanza katika kifungu hicho kuwa sehemu kubwa katika maisha yao: *'Uwe na hasira.'* Lakini tafsiri bora ya msitari ule ni, *'Wakati una hasira, usitende dhambi.'* Mungu anafahamu kwamba ni kawaida kuwa na hasira. Lakini ujumbe wa Biblia kwa waamini ni, *'hili kwamba usiruhusu hasira kukuongoza katika dhambi, na pia usiruhusu jua kutua ungali mwenye hasira.'* Kiini cha Maandiko yanayozungumza kuhusu hasira ni kwamba *'tutupilie mbali'* hasira na uchungu wote **(Waefeso 4:26-27).**

Nilipofahamu kwamba Mungu kupitia Neno lake, aliniambia nisiwe na hasira au uchungu, ilinibidi 'kutupilia mbali', swali hili langu, 'kwa jinsi gani?' Swali langu liliniongoza katika kitabu cha Mwanzo ambapo bali na kupata jibu langu, pia nilikombolewa kutoka kwa hasira. Ninakushauri utumie msitari huu ikiwa pia unakumbana na shida hii ya hasira au uchungu. Ni moja ya hadithi kuu tena mashuhuri katika Biblia.

'Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana. Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake; bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhabika sana; uso wake ukakunjamana. Bwana akamwambia Kaini, Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani walakini yapasa uishinde.'

'Kaini akamwambia Habili nduguye, Twende uwandani. Ikawa walipokuwepo uwandani, Kaini akamwinukia nduguye, akamwua. Bwana akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? Akasema, umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi' **(Mwanzo 4:3-10).**

Katika hadithi hii fupi, tunapata mafundisho makuu kuhusu hasira au ghadhabu. Kuna watu, aliyekubalika (Habili) na asiyekubalika (Kaini). Wote wawili waliyafanya matoleo kwa Mungu. Kwa hakika, Mungu alipendezwa na sadaka ya Habili, lakini hakupendezwa na ya Kaini. Siamini kwamba tumepewa maelezo ye yote kuhusu ni kitu gani ambacho hakikukubalika kuhusu sadaka au matoleo yake Kaini. Yeye alikuwa mkulima, hivyo alileta mazao ya shamba. Hadithi hii inatuonyesha kwamba huyu Kaini hakuleta mazao yaliyokuwa bora.

Habili alikuwa mfugaji, naye akaleta wanyama. Baadhi ya watu husema kwamba shida ilikuwa kwamba matoleo yake Habili yalikuwa ni damu ya mifugo ilhali ya Kaini hayakuwa hivyo. Lakini hapakuwa na mafunzo au utaratibu wo wote kuhusu matoleo ya dhabihu au sadaka yenye damu. Naonelea kwamba mkazo mkuu upo kwa hawa watu wawili zaidi kuliko waliyotoa kama sadaka. Mmoja wao alikuwa amekubaliwa. Naye yule mwingine hakukubalika hivyo basi, matoleo yake hayakubalika.

Tukio hili linaendelea; aliyekubalika anatembea pamoja na yule asiyekubalika ambaye anampiga na kumwua. Mungu anamjia Kaini baadaye na kumwuliza, *'Mbona wewe umegadhabika? Mbona umekunjamana uso? Ndugu yako yupo wapi? Umelitenda jambo gani? Ukilitenda lililo jema je! Si utakubalika? Ikiwa hautatenda hivyo, hasira au kugadhabika huku kwako ni dhambi ambayo itakuangamiza wewe!'*

Hili ni somo kuu kuhusu kugadhabika au kuwa na hasira. Katika kisa cha redio niliyoiponda kwa konde langu, sikuwa na hasira dhidi ya mke wangu. Bali hasira ilikuwa juu yangu mwenyewe kwa kuwa nilikuwa 'asiyekubalika' kwa jinsi nilivyokuwa nimevuja vibaya fedha zetu. Hivyo basi, nilijikasirikia. Ilimbidi Mungu kuniuliza 'mbona umegadhabika? Mbona umeiponda ile redio?' Jifunze kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha zako nawe utajikubali mwenyewe na kwake Mungu au kwa ye yote yule. Ikiwa hautasuluhisha ghadhabu yako na kukubalika, utaishi maishani mwako ukivunja redio, au 'kumpiga Habili' na hilo litakuangamiza wewe!'

Mtume Paulo ana mashauri muhimu sana kuhusu swala hili katika Waefeso. Yeye aandika, *'Yeye ampendaye mkewe, ajipenda mwenyewe'* **(Waefeso 5:28).** Unaweza kuona kwamba kama ningejipenda wakati wa tukio lile la redio, ningekuwa na uwezo wa kumpenda mke wangu. Lakini kwa sababu nilikuwa nimekunjamana, nilikuwa nikilielekeza hasira na uchungu kwa mke wangu.

Nilikuwa nikijaribu kusuluhisha shida yangu ya ghadhabu, na ilitukia kwamba nilimpenda mke wangu na wanangu. Lakini, sikudhihirisha upendo wangu wakati wote kwao, hasa wakati ambapo 'Sikujipenda mwenyewe.' Wakati nilipokuwa najihisi kuwa nimegandamizwa mno kwa

sababu ye yote ile, nilikuwa sina uwezo kuudhihirisha upendo wangu kwao. Lile nililohitaji ni jukumu langu lenye haki kujitambua na kujipa heshima jinsi Mungu alivyo nitazama.

Katika kitabu cha Mathayo, mwana sheria alimwuliza Yesu, *'Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu?* **(Mathayo 22:36)**.' *Naye Yesu akajibu, 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa akili zako zote.* Hii ndiyo amri ilyo kuu, tena ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii **(Mathayo 22:37-40)'**

Yesu alikuwa akisema kwamba ni lazima tutawale mitazamo mitatu katika maisha ili kuwa na kile alichotaja kama 'uzima wa milele'. Ni lazima tutazame juu na kufanyika vile tunavyohitajika katika uhusiano wetu na Mungu. tena ni lazima tutazame ndani yetu na kufanyika jinsi Mungu anavyokusudia tuwe, ni lazima tutazame kando ili tuwe kile Mungu atuambia katika Neno lake kuhusu uhusiano wetu na watu wengine. Yesu anajumuisha mitazamo hii mitatu kwa kutufundisha kwamba tunahitajika kutazama juu, na kumpenda Mungu kabisa. Tunahitaji kutazama ndani, na kujipenda jinsi inavyostahili. Pia tunahitaji kutazama kando na kuwapenda wengine bila masharti ye yote.

Hebu ifahamike kwamba kujipenda haimaanishi kutupilia mbali ibada kila wakati wanapopita karibu na kioo. Hivi ndivyo watu wengi huifikiria. Lakini rafiki yangu, ambaye amekombolewa kutoka na janga la ulevi wa pombe na madawa ya kulevya, anajumuisha kwa njia hii: 'Mpende Mungu kabisa, jipende mwenyewe inavyostahili, na umpende mwingine bila masharti ye yote.' Huyu rafiki yangu aliweza kukua kiroho wakati alipotambua mambo haya matatu, na kwa matokeo yake, amekuwa mtu aliyemakinika bila ulevi kwa miaka kumi na saba. Sasa ndiye mwenye kiti katika baraza la wazee katika Kanisa letu.

Wakati Paulo anaposema, *'Yeye ampendaye mke wake ajipenda mwenyewe,'* huwa anatujulisha siri. Usipopenda wakati unatazama ndani, ikiwa una ghadhabu kwa ajili ya ubinafsi kiasi kwamba unajidharau mwenyewe hata kujiangamiza, hautaweza kupatana na ye yote hasa mwenzio.

Ikiwa utashirikiana na mtu ye yote hasa katika uhusiano wa ndoa, ni lazima umfahamu. Hatuwezi kutenganisha kufahamiana na kuwasiliana kati ya watu na Mungu.

Tunawezaje Kufahamiana Mmoja Na Mwingine?

Ukweli ni kwamba, sisi wenyewe hatujifahamu kikamilifu, bali na kwamba hatuwafahamu wenzetu. Yeremia alisema, *'Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?* **(Yeremia 17:9).** Katika msitari ufuatao, sauti yake Mungu ilijibu swali lake Yeremia. *'Mimi Bwana nauchunguza moyo, . . .' (***10).** Kwa kuwa jambo hili ni la kweli, basi kama Daudi, tunahitajika kutazama juu na kusema, *'Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu,*

uyajue mawazo yangu **(Zaburi 139:23).**' Mawasiliano ya aina hii na Mungu ndio njia ya pekee ambayo tunaweza kujifahamu na kuanza kufahamiana katika ndoa. Ikiwa mmoja kati ya wawili hana mawasiliano na Mungu, kwa hakika wao hawataweza kufahamiana vyema.

Yakobo anatushauri: *'Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa* **(Yakobo 1:5)**.' Kwa maelezo mengine, inawezekana kwamba usimfahamu mwenzio, lakini Mungu anamfahamu. Wakati utakapotambua kwamba hauwezi kumfahamu bila usaidizi wa Mungu, basi mwulize Mungu akupe hekima ambayo unakiri kwamba hauna.

SURA YA PILI

Dira Ya Kiroho

Kitabu cha Mwanzo ni kitabu cha mianzo. Hii ndiyo maana ya neno Mwanzo. Katika kitabu cha Mwanzo, Mungu anatuambia kuhusu mianzo ya mambo mengi kwa sababu Yeye anataka tufahamu mambo hayo jinsi alivyokusudia. Nakala ya kwanza ya mazungumzo yake Mungu na mwanadamu imenakiliwa katika sura ya tatu ya kitabu cha Mwanzo, baada ya Adamu na Hawa kula tunda walilokatazwa. Kwa kutotii, wao walipata ujuzi wa kujua mema na mabaya, hivyo basi, wakajificha kwa kuwa walijihisi wenye hatia na aibu.

Tunasoma kwamba Mungu alifuata viumbe hawa wake wenye kuasi kote katika bustani na alipowapata, aliwauliza maswali. Muumba anapouliza viumbe vyake maswali, sio kwamba yeye hafahamu majibu yake. Kusudi lake Mungu kuuliza maswali ni kumfanya mwanadamu kufikiria. Maswali haya ya Mungu ni kama 'dira ya kiroho.' Kwa sababu ndoa ni kuanza na watu wawili katika ndoa, ningependa kushiriki maswali manane ambayo Mungu anatuuliza katika Biblia ambayo yanaweza kuwasaidia watu walio katika ndoa kujifahamu wenyewe na kuwafahamu wenzi wao.

Maneno ya Mungu ya kwanza kwa mwanadamu aliyeanguka katika Biblia ni: *'Uko wapi?* **(Mwanzo 3:9)'** Hii inamaanisha, *'wewe unahitajika kuwa mahali fulani lakini hauko hapo. Hivyo basi, uko wapi?'* Hakika ni kwamba, swali lilikuwa, 'fikiria pale ulipo, kwa sababu haupo unapohitajika kuwa.'

Adamu akajibu, *'Nilisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha* **(10).**' Kwa maelezo mengine, *'Nilipoisikia sauti yako, niliingiwa na hofu. Nilifahamu kwamba itadhihirisha uchi wangu na sitaki kuonekana.'*

Haya ni maelezo sahihi kuhusu asili ya mwanadamu kama ilivyokuwa, na kama ilivyo siku ya leo. Je! Wakati mwingi una ushawishi kwamba unahitajika kuwa mahali fulani, ilhali hauko pale? Hebu tilia maanani kwamba ushawishi ule unaweza kuwa ni Mungu anayekuuliza hivi, 'Uko wapi?' Je! Inawezekana kwamba kile tunachotaja kama 'pingamizi la kujifahamu mwenyewe' ni kile Mungu anachotueleza katika sura hii ya tatu kitabu cha Mwanzo? Je! Inawezekana kwamba Mungu anataka tufahamu jinsi ilivyokuwa miujiza ambayo Muumba wetu anatutafuta siku ya leo kwa maswali yanayozolea mahali tulipo, kwa sababu hatuko pale anapokusudia tuwe?

Swali la pili ambalo Mungu anamwuliza mwanadamu ni, *'Ni nani aliyekuambia?'* Kwa ufafanusi, *'Ni nani aliyekuambia kuwa u uchi?* **(11).'** Katika lugha ya Kiebrania alisema hivi, *'Ni nani aliyekufanya wewe kufahamu kwamba u uchi?'* Swali hili la pili la Mungu linamwelekeza Adamu na Hawa nyuma pale walipo kula tunda kutoka kwa mti waliokatazwa. Wao walipokula kutoka

kwa mti waliokatazwa, tunasoma kuwa, *'Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mitini, wakajifanyia nguo* **(7).'**

Sasa Mungu anauliza, *ni nani aliyekufanya kujua kwamba ulikuwa uchi?* Jibu ni kwamba Mungu mwenyewe aliwafanya wao kujua kwamba wako uchi kwa kuwa anawapenda. Mazungumzo haya ya Mungu pamoja na Adamu na Hawa, ni maelezo yenye kuvutia ya upendo Wake, kama ilivyokuwa na ilivyo sasa. Ni Mungu aliyewafungua macho kwa sababu alitaka viumbe vyake kufahamu yale waliyotenda, na kufanya tendo kuhusu kweli kwamba wao hawakuwepo mahali walipostahili kuwa. Mungu hudhihirisha upendo Wake kwetu kwa njia ile ile hata siku ya leo.

Swali la Mungu la tatu na la nne litatuongoza katika toba. Swali la tatu lilikuwa ni hili: '*Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?'* Ni maoni yangu kwamba miti hii ilikuwa mifano. Simaanishi kwamba hizi ni hadithi za ngano au hekaya ambazo hazina maana. Mfano katika hadithi ambayo kuna watu, mahali na vitu, vina maana zaidi na kwa wakati mwingi ni mafunzo yenye tabia njema au maana kuu ya kiroho. Je! Wewe umewahi kuona mti wa hekima? Je! Umewahi kuona mti wa uzima? Je! Umewahi kusikia au kuona sauti ikitembea? Lazima hii ni hadithi inayotumia lugha ya mafumbo. Lakini ni kweli gani ambayo tunafundishwa katika hadithi hiyo?

Katika hadithi hii ya mafumbo kuhusu miti, Mungu kwa urahisi anasema: *'Mimi nilikuweka uliwmenguni huu nami nafahamu mahitaji yako vyema zaidi ya vile unavyofahamu. Mimi ninaweza kukutana na mahitaji yako kupitia miti hii ikiwa utakula kutoka kwake jinsi Mimi nitakavyokuongoza kukutana na mahitaji yako kupitia miti hii.'*

Tunasoma kwamba Mungu alichipusha miti kwa utaratibu wa umuhimu wake **(Mwanzo 2:8-9).** Kwanza, miti ile ilihitajika kutimiza mahitaji ya macho. Katika Biblia, macho humaanisha akili, au jinsi wewe unavyotazamia mambo. Kwa hakika Yesu alituambia, *'Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!* **(Mathayo 6:22-23).** Mtazamo wetu wa mambo ni muhimu sana. Kulingana na Yesu, jinsi tunanvyotazama mambo hufanya tofauti kati ya mwili uliojaa nuru na mwili uliojaa giza. Hapa katika kitabu cha Mwanzo, Mungu anatuzungumzia kwa mafumbo, *'Haja kuu ulio nalo Mimi kukuonyesha jinsi ya kutazamia mambo.'*

Mungu alisema kwamba miti iliyo katika bustani itatimiza mahitaji yao ya chakula. Hii inawakilisha yote ambayo mwanadamu anahitaji au anataka. Kwa njia ya mafumbo, haya yanasema jinsi Yesu angesema karne nyingi baadaye: *'Mwanadamu hataishi kwa mkate peke yake, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa chake Mungu* **(Mathayo 4:4).**' Unaweza kuona kwamba, ikiwa kwanza tunaweza kumruhusu Mungu kutuonyesha jinsi mambo yalivyo, mahitaji yetu mengine yangekuja kupitia kile miti hii inachokiwakilisha.

Wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi, wao walivunja umuhimu wa kwanza wa miti. Kwanza, wao walikula kutoka kwa mti uliokatazwa, kwa sababu ulikuwa mzuri kwa chakula, kisha kwa sababu ulikuwa wa kuvutia kwa macho **(Mwanzo 3:6).** Kuasi huko kwa taratibu za muhimu na za kwanza zake Mungu kulisababisha kufukuzwa kwao katika bustani la Edeni. Tukikataa kutawaliwa na kuongozwa na Neno lake Mungu ambalo hutuonyesha jinsi ya kuishi pamoja katika ushirika, kuasi kwetu dhidi ya kanuni hizo muhimu za kwanza siku ya leo kunaweza kutuongoza katika kutumia mabomu na zana za kitonoradi, na hata kuendeleza vita vya maangamizi katika ulimwengu huu.

Katika mafumbo haya makuu yenye uvuvio, Mungu anasema, '*Mimi nimeweka mwanadamu katika ulimwengu huu nami nisingelipenda kama yeye angeliranda-randa ovyo katika giza. Nimempa Neno langu, lakini wakati atakaposikia sauti yangu kupitia Neno langu, Sauti yangu itamfanya kuwa na raha. Yeye atajificha kutoka kwangu na kwa kweli ya Neno langu.' Basi swali la Mungu, 'Je! Umekula kutoka kwa mti mbaya?' maana yake ni, 'Je! Unaangalia sehemu mbovu ya majibu yako?'*

Labda unaweza kuuliza hivi, ‘Hili lina uhusiano gani na ndoa?’ Hii inajumuika moja kwa moja katika mazungumzo yetu ya Kibiblia kuhusu ndoa. Je! Unaweza kukumbuka hapo mwanzo katika masomo haya ya jamii na ndoa, niliibuka na maeneo manne yenye shida katika ndoa ambayo ni:

- Shida ya kwanza ni mume;
- Shida ya pili ni mke;
- Shida ya tatu ni mume na mke, na
- Shida ya nne ni watoto.

Nilionyesha kwamba mahali pa kuanzia katika kuendeleza ndoa yetu ni kati ya watu wawili wanaoifanya ndoa, hasa kwa mtu yule anayeweza kufanya kitu fulani, ambaye anawajibika - wewe binafsi.

Majibu sahihi kwa maswali haya huyafanya kuwa ‘dira ya kiroho’ ambayo inaweza kumsaidia mume na mke kuwa pale wanapohitajika kuwa na hii itawaongezea afya, nguvu, na uthabiti katika uhusiano wao katika ndoa ile.

Kabla yetu kulifikiria swali linalofuatia, nina swali ambalo ningetaka kukuuliza kuhusu ndoa na jamii yako. Je! Wewe unapata mwongozo wa ndoa yako katika desturi mila au katika Maandiko? Njia nyingine ya kuliuliza swali hili ni, ‘Je! unakula kutoka kwa mti uliokubalika au kwa mti mbaya huku ukitafuta nakala ya ndoa yako?’ Swali lingine ni, ‘ikiwa unapata nakala yako ya ndoa kwa desturi na mila, je! Ndoa na jamii yako ni imara kiasi gani?’

Zaburi ya Kwanza inaeleza kile Biblia inachotaja kama ‘Mtu aliye heri au aliyebarikiwa.’ Neno ‘heri’ linamaanisha ‘furaha.’ Jambo la kwanza ambalo tunawambiwa kuhusu huyu mtu aliye na furaha ni kwamba yeye amebarikiwa kwa kuwa mtu, *‘asiyekwenda katika shauri la wasio haki (1).*’ Je! Wewe unaenda katika mashauri ya wasio haki? Kwa mfano, unapokumbwa na shida, je! Unaenda katika mashauri ya Mungu kutoka kwa mchungaji wako au kiongozi mwingine wa kiroho katika Kanisa lako, au mtu mcha Mungu mwenye kufahamu Maandiko? Au wewe humwendea mtu asiye wa kiroho wa ulimwengu?

Nilipokuwa bado mwanafunzi katika seminari, wakati mwingi nilikuwa nikichukua mikopo ya wanafunzi. Katika benki ambapo tulichukua mikopo ile, kulikuwa na ishara moja iliyouliza: ‘Ikiwa wewe ni mwerevu, mbona wewe si tajiri?’ Na kama wanafunzi wa seminari, tulifikiria kwamba tunafahamu mambo yote! Lakini ishara ile ilitupa changa moto. Ni kwa sababu gani tulikuwa maskini ilhali tulikuwa werevu?

Wengi wetu tunahitajika kutilia maanani swali hili: ikiwa sisi tu werevu, mbona hatuna furaha? Mbona hatuna ndoa na jamii yenye furaha? Labda hatufahamu Biblia vyema. Ikiwa tuna furaha, na jamii iliyo kielelezo, kwa neema yake Mungu sisi ni mume na mke waliobarikiwa na tuna ndoa na jamii iliyobarikiwa. Na ikiwa hiyo sio hali yetu, tunahitajika, kibinafsi, kuliendea Neno la Mungu na kumruhusu kutuuliza maswali hayo.

Labda ndoa na jamii yetu haibarikiwi kwa sababu tunaenenda katika mashauri ya wasio haki wakati tunahitajika kurudi kwenye kanuni za ndoa na jamii ambazo zimedhihirishwa katika Maandiko. Ikiwa tutaendelea ‘kula kutoka kwa miti miovu’ basi ndoa na jamii yetu haitabarikiwa na Mungu.

Kurudia maswali haya makuu, swali la nne ambalo Mungu aliuliza, ambalo lilitia mwangaza zaidi kukiri ambako Mungu alitoa kwa Adamu na Hawa kupitia swali la tatu, lilikuwa, *‘Nini hili ulilofanya?* **(Mwanzo 3:13).**’ ‘Kukiri’ ni neno lenye kuunganishwa katika Maandiko, ambalo linaunganisha maneno ya kuzungumza na kufanana. Maana kamili, ‘kulizumgumza neno linalofanana na lile Mungu amelizungumzia kuhusu dhambi yetu,’ au, ‘kukubaliana naye Mungu.’ Hili ndilo Mungu analolitenda wakati anapomwuliza Adamu na Hawa, *‘Nini hili ulilofanya?’* Yeye anafahamu kwa uhakika yale ambayo walitenda, lakini angependa kusikia wao wakisema yale ambayo Yeye anafahamu. Kwa kawaida, hayo si kwa faida Yake, bali kwa faida yao.

Tunapokiri dhambi zetu kwa Mungu, huwa hatutambui jambo lile asilolifahamu. Si kwa faida ya Mungu kwetu kukiri dhambi zetu, ila ni kwa ajili ya wokovu wetu. Hakuna ye yote aliye mkamilifu wala hakuna ndoa zilizo kamilifu. Kibinafsi, na pamoja katika ndoa, tunahitajika kumruhusu Mungu kutuuliza swali, *'Nini hili ulilofanya?* Kisha kusema kile ambacho Mungu anasema kuhusu yale tuliyotenda. Tuna ahadi yake Mungu kwamba ikiwa tutakiri dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu kwa Neno lake na atatusamehe yale tuliyotenda, na yale ambayo hatukuyatenda katika ndoa zetu **(1 Yohana 1:9).**

Swali la tano linapatikana baadaye katika Kitabu cha Mwanzo, wakati Malaika wa Mungu anapomtafuta Hajiri, yule mjakazi aliyetoroka Abramu na Sarai. Yule Malaika alimwuliza hivi, *'umetoka wapi, nawe unakwenda wapi?* **(Mwanzo 16:8).'**

Sifahamu ikiwa unatilia maanani zaidi kuhusu mapenzi ya Mungu kwa maisha na ndoa yako, lakini ikiwa unatenda hivyo, hili ni swali njema ambalo unamruhusu Mungu kukuuliza mara kwa mara. Hii ni aina ya swali ambalo tunahitajika kumruhusu Mungu kutuuliza siku za mwisho kila mwaka kabla ya kuanza mwaka mpya. Na kuhusu ndoa zetu, swali hili ni njema kuthibitisha wakati wetu wa maombi ya kibinafsi tunapozungumza na Mungu kuhusu sherehe zetu za kila mwaka za ndoa.

Kina kikuu cha swali hili ni kwamba ikiwa hatuna pingamizi lo lote, basi tutaenenda kule tulikotoka. Tutaendelea kupata ujuzi ule ule ikiwa hakuna tukio lo lote litakalotokea. Je! Umewahi kufika mahali katika maisha yako ambapo unafikira kurudia mambo uliyopitia yenye kukatisha tamaa?

Biblia haitushauri kujibadilisha wenyewe, ila hutuamuru kukutana na masharti fulani kisha kumruhusu Mungu kwa kutubadilisha. Yesu anatuambia kwamba ni lazima tuzaliwe mara ya pili **(Yohana 3:3-5).** Lakini hatuambiwi kwamba tujizalishe wenyewe katika uzao wa kiroho. Kuzaliwa ni ushuhuda ambao anayezaliwa hatendi lo lote. Sisi huzaliwa siku fulani katika mwaka fulani. Kuzaliwa kwetu ni tukio lililotukia. Hivi ndivyo ilivyo katika kuzaliwa kwetu kiroho. Sisi tumezaliwa mara ya pili. Tumebadilishwa kwa kufanywa upya katika nia na mawazo yetu **(Warumi 12:1,2).**

Wafuasi wa Kristo waliozaliwa mara ya pili ni watu waliobadilika, ni watu ambao wanabadilika na kusonga kuelekea katika uzima wa milele wakati watakapobadilishwa **(2 Wakorintho 5:17; 3:18; 1 Wakorintho 15:51).** Kweli kwamba tunaweza kubadilishwa yamaanisha kwamba hatuhitajiki kuenenda ambapo hatuhitajiki au kurudi tulipotoka katika safari yetu ya maisha na imani. Yaliyopita hayafanyi maisha yetu ya wakati huu na ule ujao kubandilika. Sio lazima tuishi katika mambo yale yale siku baada ya nyingine. Ikiwa wewe hauwezi kuvumilia wazo la miaka mingine kumi kama ile iliyokutangulia katika ndoa yako au katika ujuzi wako kimaisha, mwambie Mungu, na umwulize kufanya mabadiliko ambayo yatajaza wakati huu na ule ujao kwa tumaini na wema usioweza kuzimika.

Swali lingine la sita katika Kitabu cha Mwanzo ambalo tunahitajika kulijibu mbele zake Mungu, kibinafsi, na pia kama wenzi katika ndoa. Swali hilo ndilo hili, *'U nani wewe? (***Mwanzo 27:18,32).**' Na katika fumbo lingine kuu, Yakobo pamoja na Esau waliulizwa swali hili. Yakobo akasema uongo na Esau akalia kwa sauti kuu wakati anapoulizwa, *'U nani wewe?'*

Swali hili linaulizwa mara kadhaa katika Biblia. Katika sura ya kwanza ya Injili ya Yohana, swali linaulizwa kwake Yohana Mbatizaji, aliyemtangulia Kristo duniani. Viongozi wa kidini walimwuliza, *'U nani?' Tuwape majibu wale waliotupeleka. Wanenaje juu ya nafsi yako?* **(Yohana 1:22).'**

Yohana akajibu Isaya: *'Akasema, Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, Inyosheni njia ya Bwana! (23).'* Lilikuwa jibu rahisi, na dhahiri. Yeye angeweza kusema, *'Huyu ndiye mimi, hiki ndicho*

mimi, na hapo ndipo mimi nilipo. Na ni vigumu zaidi kwangu mimi kuwa zaidi ya hivyo. Wala siwezi kujifikiri mimi kuwa kitu kingine chini ya hicho. Mimi ndiye, na pale ambapo nastahili kuwepo.'

Yesu alimwambia Yohana Mbatizaji kuwa ndiye aliyewahi kuwa mkuu kati ya wanadamu waliopata kuishi. Ni jambo gani lililomfanya kuwa mkuu? Kwa urahisi kabisa, yeye alijifahamu alikuwa nani, na pia alifahamu kile hakuwa. Yeye alikubali jukumu, wajibu na uwezo aliopewa na Mungu, kwa kuwepo alipohitajika kulingana na mpango wake Mungu. Lakini pia alikubali vipimo vya kiwango chake. Yeye alifahamu jibu lililokuwa sahihi wakati alipoulizwa, *'u nani?'*

Je! Wewe unafahamu u nani? Una yapi uwezayo kusema kujihusu? Wakati watu wawili walio katika ndoa moja mbele zake Mungu wanapohitaji kujenga na kutia nguvu ndoa yao, wao wanahitajika kuanza kwao wenyewe. Ndoa yao itakuwa yenye furaha na kutimilika jinsi ambavyo wenye kuhusika kibinafsi walivyo mbele zake Mungu. Wakati kila mmoja binafsi anapoweza kusema jinsi Yohana Mbatizaji alivyosema kujihusu, wao wana mawe ya kujenga msingi wa ndoa bora pamoja na jamii yenye furaha.

Punde tu unapogundua kwamba Mungu anapenda kuuliza watu wake maswali, utampata Akitenda hivyo kote katika Agano la Kale na Jipya. Yesu anauliza maswali matatu katika Injili ya Mathayo. Unapozidi kutembea na Mungu, mpatie fursa akuulize maswali haya unapozidi kusoma Biblia yako.

Swali la saba ni, *'Wewe ni nini?'* Hili ni swali ambalo linatoka katika maneno haya ya Mtume Paulo: *'Lakini kwa neema yake Mungu nimekuwa hivi nilivyo*. . **.(1 Wakorintho 15:10)**.' Yeye pia alizidi kuandika kwa Wakorintho: '.....*Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo ulipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?* **(1 Wakorintho 4:7)**.' Kile tulicho kinahusiana na uwezo wetu wa asili na wa kiroho, karama zetu, na vipawa vyetu na hii hutangaza huduma zetu. Vitu hivi vyote hutoka kwake Mungu ili kutuwezesha kuwa kile Mungu anataka tuwe pamoja na kuwa mahali ambapo yeye anataka tuwepo.

Agano la Kale linaanza Mungu akiuliza, 'Uko wapi.' Ilhali Agano Jipya linaanza na mamajusi wakiuliza, *'Yuko wapi yeye? (***Mathayo 2:2).'** Injili yake Yohana inaanza Yesu akiuliza swali la nane. *'Mnatafuta nini?' au 'mnataka nini?* **(37).'** Wakati Yesu alipouliza swali hili la nane, Alikuwa akiwasilisha maswali mawili ambayo kila mmoja wetu anahitajika kujibu: je! Sisi tunahitaji kuwa wale, au kuwa pamoja na pale Mungu anataka tuwepo, na ni kwa jinsi gani tunahitaji majibu sahihi kwa maswali haya?

Shauku Yetu Kuu

Maswali haya manane katika Maandiko yanatuelekeza kwenye ukweli mkuu wa kiroho. Kuna mahali ambapo Mungu anataka tuwepo katika maisha haya. Kuna aina ya mtu ambaye Mungu anataka sisi kuwa. Kuna kitu ambacho Mungu anataka sisi kuwa na kitu ambacho tutafanya humu duniani. Wakati Kristo aliyefufuka na anayeishi anapoingia maishani mwetu, kama Mtume Paulo, shauku yetu kuu inahitaji kukamata kusudi ambalo Yeye ametushikia. Swali letu la kila siku kwake Yeye linahitaji kuwa, *'Bwana, wewe wahitaji mimi kutenda jambo gani?'* Mahali ambapo tutapata furaha ni katika kile Paulo alichotaja kuwa, ' ..mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu **(Warumi 12:2).**' Katika mapenzi kamili ya Mungu, sisi hupata pahali petu, na kutambua utu wetu, pamoja na mwito wetu wa kipekee.

Dira Ya Kiroho

Kuna maelekeo nane katika dira, mimi naona haya maswali manane kuwa dira yangu ya kiroho. Huyatazama mara kwa mara. Maswali haya hayabadiliki, ila majibu hubadilika kila wakati. Kuna majibu manane kwa maswali haya, na hakuna mmoja kati yenu atakuwa mwenye furaha hadi utakapopata majibu yake. Yajadilie maswali yale na mwenzio, na kushiriki pamoja jinsi unavyohisi kuhusu majibu yake kwako kama mwaminifu wa kibinafsi, na kama walio katika ndoa na jamii.

Kulingana na ujuzi wa miongo mitano ya kuwashauri wenzi waaminifu, uvumbuzi wangu ni kwamba ikiwa Mume au mke hana furaha, ushirika wao hautakuwa wenye furaha. Sababu moja iliyo kuu ya kutokuwa na furaha miongoni mwa waaminifu ni kutokuwa na majibu sahihi kwa maswali haya yake Mungu sawa na mengine kama yale.

Kukupa changa moto kama wenzi walio katika ndoa, kufuatilia mawasiliano yaliyo katika maeneo yenye upana mkuu kwa kujibu maswali haya mbele zake Mungu na kujadiliana mmoja kwa mwingine. Kisha kwa uangalifu mkuu sikiliza majibu ya mwenzio. Ikiwa utatenda hivi, utashangazwa kwa yale Mungu anaweza kutenda katika maisha yenu.

Ni janga kuu kwa mwaminifu kuishi maisha bila kufikiria mambo haya. Waaminifu wengi huishi maisha yenye kushindwa na hawalifahamu jambo hili. Ikiwa haujatosheka na thamani ya maisha yako ya kiroho, kwa makini tafakari maswali haya kana kwamba Mungu ndiye anayekuuliza. Maswali haya na majibu yake yanaweza kubadilisha maisha yako kuelekea upande mwingine. Wakati hili linapotukia kwake mume au mke mwaminifu, utimilifu wao wa kibinafsi katika Kristo huwabadilisha na kuyaingiza maisha katika ndoa yao.

SURA YA TATU

Furaha Ya Kudhihirisha Umoja

Tunasoma katika Kitabu cha Mwanzo kwamba Mungu alitazama kila kitu alichoumba na kusema, *'ni vema!'* lakini aligundua kitu ambacho *'si vema.'* Yeye asema, *'Si vema huyu mtu awe peke yake* **(Mwanzo 2:18).**' Hivyo basi, Mungu alimfanyia msaidizi wa kufanana naye Adamu, na wao wawili walifanyika 'mwili mmoja.'

Jambo la kwanza ambalo tunahitajika kutambua kuhusu uumbaji wa Mungu wa uhusiano wa ngono ni kwamba Mungu alikusudia kwamba ngono iwe kwa uzazi. '*Zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi.....'* Yeye aliwaamuru Adamu na Hawa **(Mwanzo 1:28).** Tumejifunza kwamba ndoa ni mpango wa Mungu kuijaza dunia kwa watu wema. Yeye hataki tujaze watu tu, bali tufanye hivyo kwa watu wema. Ili jambo hili litimie, wazazi ni lazima wawe thabiti, na wakamilifu. Pia ni lazima wawe wenzi wenye nguvu pamoja ili hatimaye wawe na nguvu kama wazazi na kuzaa watu wenye nguvu kupitia ndoa na jamii yao. Ni dhahiri kwamba, Mungu alikusudia ngono kutumika kwa hali ya kijamii na katika ndoa, na kwamba Alikusudia iwe kwa ajili ya uzazi.

Na zaidi ya uzazi, Mungu alikusudia ngono iwe chombo cha kudhihirisha wenzi walio kwenye ndoa. Wakati wenzi wanapokuwa na shida ya ngono, kabla ya kutazamia juu ya shida hiyo, wanahitaji kwanza kuchuguza hali ya umoja wao wa kiroho. Wanahitaji kufikiria kuhusu mawasiliano yao pamoja na maeneo mengine ya utangamano. Wao wanahitaji kuchunguza thamani za kweli, zenye upendo unaofanana na ule wa Kristo pamoja na mambo ambayo yanahusika katika kufahamiana kati yao. Hapo tu ndipo wao wanaweza kukumbana na shida ya kiroho.

Ni dhahiri kabisa kwamba ngono, ambayo ni mpango wa Mungu kwa ajili ya kudhihirisha furaha ya umoja wetu, inaweza kufanyika kuwa kuzuizi katika umoja wetu. Ikiwa dhihirisho la kimwili kwa umoja wetu ni kile Mungu alichopanga kuwa, basi inawezekana kuwa asilimia kumi ya uhusiano. Lakini ikiwa uhusiano wa kimwili haumo katika mpango wake Mungu, inaweza kuwa asilimia tisini ya shida. Ndoa huvunjika kwa sababu ya ngono, na ikiwa mmoja katika ndoa ile hatosheki. Hivyo ni kitambo kidogo kabla hawajapata mtu mwingine kando ambaye atawatimizia.

Kinyume ni kwamba kile Mungu alichoumba kwa ajili ya kudhihirisha umoja wetu kinaweza kuwa mojawapo ya kikwazo kikuu katika umoja ule. Ni yule mwovu peke yake

anayeweza kukichukua kile Mungu alichotayarisha kuwa dhihirisho ya furaha ya umoja wetu na kukifanya kuwa mojawapo ya vikwazo vikuu kwa umoja wetu.

Wakati ngono ni asilimia tisini ya shida kati yake mume na mke, haja lao kuu la kwanza linafaa kuwa: Wao huwa wanadhihirisha nini wakati wanapojamiiana? Ikiwa hakuna umoja wa kiroho, mawasiliano, upendo, na kufahamiana, wao huwa wanadhihirisha nini? Ikiwa hawana moja kati ya maeneo haya ya uhusiano, ngono inawezaje kuwa ile Mungu aliyoumba? Ikiwa wao hawana umoja wa kudhihirisha, uhusiano wao wa ngono ni sawa na ule wa wanyama wa mwituni.

Unapoingia katika tendo hili la umoja katika ngono, je! Umejitolea kikamilifu kumtosheleza mwenzio? Hii ndiyo aina ya kujitolea ambayo huifanya ngono kuwa ilivyokusudiwa na Mungu. Kwa maelezo mengine, bila mawasiliano ambayo ni ‘kiunganishi cha upendo,’ ambacho Mungu alitayarisha kwa ndoa, wao hawataweza kuwa na uhusiano wa ngono ambao Mungu alioutaja kama ‘mzuri zaidi.’ Hata kwa njia nyingine, kiwango chao cha umoja wa kiroho kitaamua thamani ya ushirika wa kimwili walio nao katika ndoa.

Mungu alikusudia ngono iwe kwa ajili ya uzazi na pia kama chombo cha kudhihirishia wenzi walio oana, lakini pia. Alikusudia kwamba ngono iwe kwa ajili ya ridhaa au raha. Haijulikani ilianza wakati upi. Watu wengi wanaamini kwamba ilikuwa ni wakati wa enzi au miaka ya uongozi wa *Victoria* huko Uingereza. Lakini, zamani za kale, Wakristo walikuwa na dhana kwamba raha ya ngono ni nzuri. Kwa mtazamo wao, Mungu hakuhusika na cho chote kuhusu ngono.

Siwezi kutilia uzito wa kutosha juu ya jinsi ilivyo muhimu kulivuka wazo hili lisilo la Kibiblia. Wakati mwanamume na mwanamke wanapo amini kwamba ngono si nzuri au kwamba ni mbaya, inawezekana kwamba wana ubaridi au shauku katika ndoa. Ngono ni safi. Ni takatifu. Sisi hatuhitajiki kuamini mengine au kuwapa watoto wetu mawazo mengine. Hii ni changa moto, kwa hakika. Ikiwa unataka mwanao wa kiume na kike kuwa bikira wakati anapofunga ndoa, kwa hakika ni vigumu kumfanya kujizuia bila kufikiria kwamba kuna jambo mbaya katika ngono.

Katika maelezo ya uumbaji, Biblia inatuambia kwamba ngono ni njema. Kitabu cha Wimbo Ulio Bora, kwa mfano, ni mojawapo ya vitabu vyenye kuvutia katika Biblia. Kwa maoni yangu, kusudi lake katika vitabu vya Maandiko vilivyokubalika kwamba ngono ni nzuri na iliumbwa na Mungu. Ni vyema sana kuwa uhusiano wa ngono jinsi unavyoelezwa katika kitabu cha Wimbo Ulio Bora. Pia kuna mafumbo mahali pale. Ni picha ya upendo wake Kristo kwa Kanisa, na Mungu Yehova kwa Israeli. Lakini hayo ni matumizi ya ziada. Matumizi ya kwanza ya kitabu hiki ni kutuonyesha kwamba ngono ni nzuri.

Ngono huvutia. Imeumbwa na Mungu hili iwe takatifu, safi, nzuri na dhihirisho la furaha la upendo kati ya mume na mke. Dhana ye yote kuhusu ngono katika hali ya ndoa ambayo haiambatani na maelezo yale ya kitendo hicho haitoki kwa Mungu, bali kwa yule muovu.

Je! Matarajio yako pamoja na utu wako pale ambapo pahusika na umoja katika ndoa ni yapi? **Kumbukumbu la Torati 24:5** inaeleza sheria ya Kiyahudi ambayo iliamrisha nyakati zenye raha kuu kwa wenzi waliooana *‘Mtu atwaapo mke mpya, asiende vitani pamoja na jeshi, wala asipewe shughuli juu yake yo yote; akae faragha mwaka mmoja nyumbani mwake, apate mfurahisha mkewe aliyemtwaa*.’ hivi karibuni:

Wasomi wengi huamini kwamba neno ‘apate mfurahisha’ linamaanisha kwamba mumewe alitarajiwa kumfurahisha mkewe kwa njia ya ngono, kumpa raha ya ngono. Kwa

maelezo mengine, sheria iliwapa mwaka mmoja wa faragha baada ya ndoa - *(Honeymoon).* Je! Wewe unafikiria jambo hili kuwa linazungumzia jinsi Mungu anahisi kuhusu ngono?

Katika Agano jipya, kuna changa moto katika kuheshimu ndoa na kulinda usafi wake katika kukaribiana kwa njia ya ngono kati yake mume na mke. *'Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana washerati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu* **(Waebrania 13:4).'** Hapa Mungu anaibagua ngono isiyo katika ndoa, na kutilia mkazo kwamba ndoa iheshimiwe na uhusiano wake kati ya wenye kuoana unahitajika kuwa mtakatifu na safi.

Utafaidika kusoma **1 Wakorintho 7:1-7** pamoja na **Mithali 5:15-20,** pamoja na **Kitabu cha Wimbo Ulio Bora.** Tilia maanani vifungu hivi vya Maandiko, kisha ujiulize nia na matarajio yako katika ngono. Nia ni muhimu sana katika uhusiano wa ngono. Imetambulikana kwamba chombo kikuu tulicho nacho kuhusu ngono ni akili zetu.

Unaweza kutumia uhusiano wa ngono katika fumbo lile la miti lililo kwenye sura ya tatu ya Kitabu cha Mwanzo ambacho tumekielezea katika sura iliyopita. Wewe uliumbwa na haja wa ngono, lakini haja kuu ni kumwuliza Mungu kukutana na mahitaji ya macho yako, au akuonyeshe kusudi na mahali pa ngono. Ukiweka haja hiyo mbele, hakika hautakosa yote ambayo Mungu alikusudia wakati Alikupa pamoja na mwenzio hali ya kudhihirisha furaha yenu. Ikiwa utatenda kulingana na njia yake Mungu, basi utaweza kutosheleka kwa kila kitu ambacho kinapatikana katika ngono. Lakini, ikiwa utaweka tamaa ya ngono kwanza, hasa nje ya ndoa, utalipia matokeo yake.

Ni kupitia Maandiko, Mungu anatuonyesha jinsi ya kutazamia mambo. Ikiwa tutaruhusu Neno la Mungu kutuonyesha utu pamoja na matarajio yetu kuhusu ngono, basi tutagundua kwamba ngono imetayarishwa na Mungu kudhihirishwa katika mazingira ya ndoa na jamii.

Je! umepata wapi habari kuhusu ngono? Ikiwa unapata ishara zako katika mila na desturi, hautapata habari zinazoweza kukusaidia katika ndoa yenye furaha na jamii ya Kikristo. Hivyo basi, unaweza kupata wapi habari kuhusu ngono? Kutoka kwa wakufunzi? Au kutoka kwa daktari wako? Ama kutoka kwa serikali? Watu wengi husema kwamba nyumbani ndipo ngono inahitajika kufafanuliwa. Lakini ni nani ambaye anawafunza watu ambao wanazijenga nyumba zile? Na wapi ambapo walio katika ndoa waelezwa kuhusu mpango wa Mungu kuhusu ngono?

Nimeamua kwamba ikiwa Kanisa halitawaambia, basi hakuna mwingine anahitajika kufanya hivyo. Hakika ni wapi ambapo unaweza kujifunza kuhusu sehemu ya kweli na kusudi la ngono ikiwa hauwezi kufanya hivyo katika Kanisa? Ndoa ni dhana ya Mungu, na imenakiliwa katika Maandiko. Hii pia ni kweli kuhusu ngono. Wakati unaposoma Maandiko kama Wimbo ulio Bora, utatambua kwamba Mungu hayuko kimya kuhusu ngono. Hivyo basi, wahubiri hawahitajiki kuwa kimya.

Nimesema kwamba kabla ya mtu ye yote kuhubiri kutoka kitabu cha Wimbo Ulio Bora, ni lazima awe na mvi kichwani mwake. Nilipokuwa mwanafunzi katika seminari, tulikuwa na mzee mkongwe mwenye mvi aliyetutembelea kutuzungumzia kuhusu ngono. Baada ya maongezi yake ambayo yaliyokuwa ushauri na usaidizi mwingi, nilimuuliza swali hili, *'Ni wakati gani ambapo msukumo wa ngono unaanza kulegea? Ni wakati gani ambapo mwali wa moto unaanza kufifia?'* Yule mzee, tabasamu yake iliufunika uso wake wote na akasema, 'Mimi sina ufahamu wo wote ule!' Yeye alikuwa mkongwe wa miaka themanini na miwili! Hivyo basi, unaweza kuona kwamba sio lazima uwe kijana ili kufurahia raha na madhihirisho ya umoja.

Uhusiano wa ngono ulitayarishwa na Mungu hili kuleta kutosheleka kamilifu kwa ngono kati ya mume na mke. Lakini kulingana na uchunguzi wa makadirio uliofanywa, kuna wake wengi ambao hawashuhudii kutosheka huko. Ni maoni yangu kwamba sababu kuu za kutoshelezwa ni ubinafsi wa kujitakia mwenyewe bila kujali wenzetu wetu pamoja na ujinga au kutokufahamu kwa waume.

Sifa kumi za upendo jinsi zilivyoelezewa katika **1 Wakorintho 13 -** tulizotaja katika kitabu kilichotangulia - yote ni 'mambo mageni' maanake kwamba zinatokana na tofauti. Kwa kuwa sote tu wenye dhambi, kina chetu kabla ya kukujia imani ni nafsi au ubinafsi. Lakini wakati ambapo tunazaliwa kwa mara ya pili, kina chetu hufanyika kuwa Kristo, hivyo basi, kisha wale ambao huvutiwa na maisha yetu. Tunapoingia katika ndoa, kitu kingine kilicho muhimu zaidi ndani wetu ni wenzi wetu. Hili kutosheka katika ngono kushuhudiwe kwa mwanamume na mwanamke, yule mwanamume anahitajika kujali masilahi ya mwenziwe ili awe mpenzi aliyekusudiwa na Mungu.

Ni watu wenye vina vilivyobadilika tu wawezao kutosheleka katika ngono alioukusudia Mungu. Hii inamaanisha kwamba mume na mke ni lazima wawasiliane. Mume anaweza kufikiri yale anayotenda yanamfanya mkewe kuwa na utambuzi na kutosheleka, lakini hayo yanaweza kufanyika kinyume na matarajio yake. Ni lazima azungumze, amwambie, na kuwasiliana naye kwa kile anachohitaji. Watu wengi wana ushuhuda mbaya kuhusu ngono katika mazingira yao, na jambo hili linaweza kuwafanya kutosheka katika umoja wao wa ngono. Mambo haya yanahitaji kuletwa kwenye nuru ili kuleta uponyaji wa undani hivyo baadaye kutoshelezwa kwa ngono kufuatie.

SURA YA NNE

Sura Ya Ndoa Katika Biblia

Sura ya saba katika Wakorintho wa kwanza ni mojawapo ya vifungu bora katika Maandiko kuhusu ndoa. Paulo ajadili kuhusu mjadala huu huku akikumbana na maswali ambayo Kanisa la Wakorintho yalimwuliza kwenye barua yao. Unapozidi kusoma majibu haya, utapata dhana kuhusu maswali hayo yaliyoulizwa.

Katika msitari wa **26** Paulo anaandika, *'Basi, naona hili kuwa jema, kwa ajili ya shida iliyopo. . .'* Ni shida gani hii iliyokuwepo? Kwa hakika inaonekana kuwa ni dhiki iliyokuwepo. Wakristo wa kale walikuwa kila mara wakiishi chini ya tisho la dhiki hivyo basi, hili lilikuwa jambo la kukubalika kwamba ikiwa uko katika dhiki, umefungwa gerezani, au umetupwa kwenye simba, ni vyema zaidi kama usingelikuwa na mke wala watoto. Katika vizazi vingi, na katika mila na desturi nyingi, watu waaminifu, watakuwa wameiweka kando mipango yao ya ndoa hadi wakati vita na dhiki zitakapokwisha.

Waaminifu wa Korintho walikuwa wamemwuliza Paulo maswali ya aina hii, *'Je! Vijana wetu wanaweza kufanya ndoa siku ya leo, kama ilivyo wakati wa kawaida?*' Paulo alijibu, *'La! Hasha'* na mara kadhaa katika sura hii, yeye anasema, ' *Ni vyema kama mtu akikaa peke yake' akimaanisha kwamba, kulingana na mambo na shida iliyopo wakati huu.' Nao walizidi kuuliza, 'Ikiwa mtu ameufanya uamuzi kuishi peke yake, je! Wao anaruhusiwa kuwa na uhusiano wa kimwili?' Naye Paulo anawajibu kwa hakika, 'La! Hasha. Ikiwa wewe hautamtwaa mke au mume, na ikiwa nyinyi hamtaitimiza ndoa ile katika uhusiano wa ngono, hivyo basi, ni vema msiwake katika tamaa'*

Paulo anaandika, *'Kwa habari ya mambo yale mliyoandika, ni heri mwanamume asimguse mwanamke. Na ikiwa hawaoi, wasiwe katika hali ya kutangamana kimwili.'* Hii inaeleza maneno yake ya hapo mwanzoni kwamba ni vema ikiwa hawatamgusa mwanamke. Jinsi gani ya kuanza sura kuhusu ndoa! Paulo akubaliana nao kwamba ikiwa wao hawawezi kuzitawala tamaa zao, basi wanahitaji kuoa, kwa kuwa ni vyema kuoa kuliko kuwaka tamaa.

Itakuwaje kwa wale tayari wameoana? Je! Wao wanastahili kuwa na maisha ya kawaida katika ngono yao? Paulo ajibu kwenye fungu lililo kuu kuhusu uhusiano wa ngono kati ya waaminifu wawili: *'Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika, ni heri mwanamume asimguse mwanamke. Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe. Mume na ampe mkewe haki yake, na vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake. Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe. Msinyimane isipokuwa*

mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu. Lakini nasema hayo, kwa kutoa idhini yangu, si kwa amri **(1 Wakorintho 7:1-6).'**

Hiki ni kifungu kizuri sana kuhusu ushauri wa uhusiano wa kimwili katika ndoa ya Wakristo wawili. Baadhi ya mambo ya ufupisho ambayo Paulo anayazungumzia kuhusu furaha ya umoja katika uhusiano wa ndoa iliyo mbele za Mungu:

Tamaa ya ngono ni kuu, lakini ndoa ina nguvu hata kuitawala tamaa ile na kulinganisha hata kutosheleza vyema maisha ya ngono ambayo yanawalinda wenzi hawa wawili kutokana na majaribu katika kizazi hiki kiovu ambacho wenzetu katika Korintho walipata kuishi.

Mkazo wake ni kwamba, mume ni lazima amtosheleze mkewe, vile vile mke ni lazima amtosheleze mumewe. Maelezo mengine, mume ni lazima amfanye mkewe kuwa kina chake, vivyo hivyo inampasa mkewe kumfanya mumewe kuwa kina chake.

Kujitenga na ngono kunakubalika, lakini kwa muda tu kwa ajili ya kumkaribia Mungu kwa njia ya maombi na kwa kufunga. (Hii si kunatanata kuwa kichwa kinauma wakati wote.) Muhimu hapa ni kwamba uhusiano wao na Mungu ungali wa faragha na tofauti. Ingawa wao hushiriki katika hayo kwa njia nyingi, uhusiano wao na Mungu ni msingi wa umoja wao, kwani hawakushauriwa kumtafuta Mungu pamoja kama wenzi.

Dhana kuhusu makubaliano ni muhimu. Swali moja kuhusu ngono ambalo huibuka mara kwa mara katika ushauri kati ya watu waliokuwa katika ndoa kwa wakati mrefu ni 'Je! Kuna mambo maovu au yaliopotoka?' Nafikiri jibu ni kwamba hakuna mabaya kati ya mume na mke ikiwa watakubaliana na kupendezwa na maamuzi yao wawili. Swali lililo sahihi sio, 'Ni kipi kilicho chema?' ila ni 'kipi kinachokubalika kati ya wote wawili?' Watu huuliza maswali kuhusu uzoevu wa ngono lakini ulio muhimu ni hali na kadiri. Lile ambalo linahitajika kutiliwa maanani zaidi ni yale makubaliano kati ya wenzi hawa wawili.

Tambua Paulo anasema kwamba ngono ni chaguo la wahusika katika ndoa. Ni uamuzi wa kupeana raha au kumtumikia mwenzio. Wakati unapojitolea kumpenda mtu, huwa umejitolea kwa uhusiano wa kimwili. Ni kusudi lake Mungu kwa kujitolea ambako ni kwa watu wawili wasio na masharti. Ikiwa kila mtu amejitolea kikamilifu kwa raha ile, pamoja na kumtosheleza mwenziwe; huwa na ufunguo ambao unafanya uhusiano wa ngono kuendelea.

Waume kwa wakati mwingi huwaambia washauri, '*Mke wangu hana hamu ya ngono. Ninaweza kutenda nini ili kumpatia hamu hii?*' Shtuma hilo husikika kutoka kwa wake zao pia, wakisema: 'Mume wangu hana hamu ya ngono.' Kutokuwa na hamu ya ngono hutokana na kutomfanya mwenzio kuwa kina cha maisha yako kati yao.

Tayari nimegusia kwamba ni muhimu kwa mume kumfanya mkewe kina cha maisha yake. Ikiwa wewe ni mume anayekumbana na kutokuwa na hamu kwa mwenzio, jitahidi kuwa na ufahamu mwema kuhusu ngono. Kati ya mazungumzo mengi miongoni mwa wanaume wenye kujidai ndume, wengi wao huwa hawana ufahamu kuhusu sehemu za kike za wake zao. Je! Mkeo hutosheka na ngono au mshushio unapokuwa na ushirika wa kimwili? Ikiwa hatosheki, ningependa kukuuliza swali hili: Ikiwa wewe haujawahi kuwa na mshushio, hali hiyo imehadhiri uhusiano wa kimwili na mkeo vipi?

Amri kuu inatumika hapa. '*Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi wateendeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii* **(Mathayo 7:12).'** Changa moto iliyo kuu katika amri hii ni kujiweka binafsi mahali ambapo mwenzio yupo. Kama ungekuwa mwenzi huyo asiye na hamu katika uhusiano wa kimwili, ungemtaka mwenzio kutenda jambo gani? Utakapopata jibu kwa swali hilo, litende kwa sababu hii ndiyo sheria kuu ya upendo wa umoja.

Inasemekana kwamba katika nyaraka za Petro na Paulo, mfano bora wa kielelezo cha ndoa ni Kristo na Kanisa. Unahitaji kuwa na ushirika wa kiroho na wa kibinafsi kwa wahusika wawili, na hali hii inashuhudiwa katika picha ya Kristo na Bibi harusi wake, ambaye ni Kanisa. Ni umoja wa kiroho. Hivyo basi, wakati umoja wa kimwili unapohusika na makubaliano, na hauna masharti, ni lazima kuwepo kiwango cha kiroho katika uhusiano ule. Kiwango hicho cha kiroho hakina kujipenda wala kujitakia mwenyewe, bali huwafanya wenzi kuwa na kina kimoja cha upendo Wake Kristo anayeishi.

SURA YA TANO

Maajabu Saba Ya Kiroho Ya Ulimwengu

Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa katika chakula cha mchana na mwungwana mmoja, ambaye alikuwa akiniambia kwamba Kanisa lake lilikuwa limemteua na kumfanya kuwa mzee na mwenye kiti wa baraza kuu la Kanisa lao. Baadaye akasema, *'Je! Unaweza kudhania juu ya tukio hili, kwamba mimi hata sijakuwa Mristo!'*

Naye mtu mwingine aliyekuwa pamoja nasi katika maankuli hayo akamwambia hivi, *'Wewe huwezi kufanyika mzee wa Kanisa la huyu ikiwa wewe si Mkristo.' Naye akajibu, 'Basi wewe ndiye mtu ambaye nimekuwa nikimtafuta maishani mwangu kwa muda mrefu. Na ningependa kukuuliza wewe swali. Mkristo ni Nani?'*

Baada ya kunena naye kwa muda wa dakika tano, alitazama saa yake na kusema, *'Naam, Mimi nimekuuliza saa, nawe wanieleza jinsi ya kuijenga saa. Je! Hakuna njia nyingine ambayo unaweza kunieleza jibu sahihi na lililo nyepesi kwa swali langu?'*

Mungu alimtumia yule mtu kunionyesha kwamba nilihitaji kujitayarisha vyema hili kujibu swali lile. Hivyo basi, niliandika nakala fupi niliyoipa jina, 'Maajabu Saba ya Kiroho Ya Ulimwengu.' Lengo langu lilikuwa kuwaeleza watu wa ulimwengu kile walichohitaji kujua na kutenda hili kushuhudia wokovu.

Jinsi nimeshiriki nawe kuhusu ndoa imetukia kwangu kwamba yote hayawezekani ikiwa wewe si mwanafunzi wa Yesu Kristo aliyezaliwa mara ya pili. Yesu alisema kwamba hatuwezi kuwa washiriki wakamilifu bila msaada wa Mungu **(Mathayo 19:3-11).** Sulemani alituambia kwamba hatuwezi kuwa wazazi watimilifu bila usaidizi wa Mungu **(Zaburi 127).** Ujumbe uliopo katika Biblia yote ambao umetiliwa mkazo mkuu na Yesu, ni kwamba hatuwezi kuwa watu watimilifu bila usaidizi wa Mungu **(Yohana 3:6,7).** Siwezi kumaliza mafunzo haya bila kukueleza kile unachohitaji kufahamu na kutenda hili kuzaliwa mara ya pili. Hivyo basi, ninamalizia na 'Maajabu Saba Ya Kiroho Ya Ulimwengu.'

Ajabu ya kwanza ni lile ambalo nalitaja kama, 'Mtindo mkuu kuliko yote katika ulimwengu.' Ikiwa utautazama ulimwengu huu kupitia darubini, kwa hakika utapigwa na butwaa kwa yale utashuhudia. Lakini, muhimu ni mpangilio ambao Mungu anao kwa kila mwanadamu aliyezaliwa katika ulimwengu huu **(Warumi 12:1,2; Zaburi 139:16).**

Kila mtu aliyeumbwa na Mungu ni wa kipekee. Je! Si ni jambo la kushangaza sana kwamba kuna yamkini vidole bilioni sitini katika ulimwengu huu, na hakuna hata viwili miongoni mwao ambavyo hufanana kwa alama zake? Kwa sasa, katika tekinolojia, kuna vyombo vyenye usanifu mkuu, kiasi kwamba vinaweza kutofautisha sauti ya kila mmoja wetu bila kukosea kwa kuwa hakuna mtu awezaye kuzungumza jinsi unavyozungumza ulimwenguni kote. Na sasa, kupitia tekinolojia ya asili ya viini vyake binadamu (DNA), kila mtu anaweza kutambulika na kuthibitishwa kwenye mahakama. Na ikiwa miujiza wa utu wetu wa kipekee unaweza kuthibitishwa kwa njia dhahiri kama, je! Ni vigumu kuamini kwamba Mungu aliyetuumba katika hali hii ya kipekee, ana mpango wa kipekee kwa maisha ya kila mmoja wetu? Kulingana na Biblia, Mungu ana mpango wa aina hii na mpango huo ndio mojawapo ya maajabu saba ya kiroho ya ulimwengu.

Labda unashangaa na kusema, 'Ikiwa Mungu ana mpango katika maisha ya mwanadamu, mbona watu hawana furaha, na mbona ulimwengu wetu umejaa fujo, vita, shida na matatizo mengi? Swali lako linajibiwa na ajabu ambayo tunalitaja kuwa 'talaka kuu ulimwenguni.' Talaka ni janga kuu katika mila na jamii tofauti ulimwenguni siku ya leo, ingawa iliyo kuu ulimwenguni ni kati ya mwanadamu na Mungu.

Biblia inatuambia kwamba Mungu alimuumba mwanadamu kama kiumbe chenye uchaguzi. Alikipatia uwezo wa kumwambia muumba wake, '*Wewe uliniumba mimi kwa mtindo huu, lakini mimi sitaki sehemu ye yote katika mpango huu. Mimi nitaishi maisha yangu mwenyewe kwa njia yangu mwenyewe.'* Maandiko yanatuambia hayo ndiyo mwanadamu anayomwambia Mungu. Biblia inataja hali hii kuwa dhambi. Kwa kuasi kwao, watu hujipatia talaka wenyewe kwa kuachana na Mungu, naye huwa ruhusu kutenda hivyo. Talaka hii ndiyo sababu kuu ya mchafuko tunaoshuhudia ulimwenguni siku ya leo. Kweli Mungu ametuumba kwa uwezo wa kujipatia talaka ya kuachana naye ni ajabu nyingine ya kiroho kwa ulimwengu.

Ajabu ya tatu ya kiroho ni 'Shaka kuu katika ulimwengu.' Kama matokeo ya talaka kuu ya ulimwengu, Mungu anakumbana na shida ile ile ambayo sisi hukumbana nayo kama wazazi. Sisi tunawapenda watoto wetu, na kuna baadhi ya tabia fulani ambazo tungependa kuziona ndani ya maisha yao. Tisho kuu la kutushangaza, ni wao hutenda mambo ambayo hayatupendezi. Wao huvunja mioyo yetu kwa yale wanayotenda. Wakati mambo haya yanapotendeka, sisi tunahitajika kukumbana nayo kwa njia gani? Tunataka kuudhihirisha upendo kwa watoto wetu, lakini hatutaki kufungua macho yetu kwa matendo haya. Hili ni jambo ambalo baadhi ya wazazi hushuhudia.

Mungu ana shaka sawa na hiyo (kusema kwamba yeye hukumbana na shaka ambayo hawezi kutatua). Yeye huona viumbe vyake vikimtaliki muumbaji wao na kutenda maovu ambayo yeye hakukusudia wao kutenda. Shaka katika ulimwengu ni lile ambalo Mungu hukumbana nalo kila mchana na usiku kutoka kwa jamii ya wanadamu.

Shaka hili katika ulimwengu hutatuliwa kwa yale tunayosikia katika ajabu ya nne ya kiroho - 'Tangazo kuu ulimwenguni.' Tangazo kuu ulimwenguni sio hotuba kutoka kwa taifa au serikali fulani. Tangazo kuu linapatikana katika Biblia, na linaitwa 'Injili,' au 'Habari Njema' kwamba Mungu alimtuma mwanawe wa pekee duniani hili apate kufa juu ya msalaba kwa ajili yangu na yako. Na alipotenda hili, Mungu alifanya kila kitu kilichohitajika kwa kutatua tatizo kuu na kuwaunganisha pamoja walio katika talaka kuu ulimwenguni. Unapofahamu tangazo hili kuu, utatambua kwamba msalaba wa Yesu Kristo kwa hakika ndio ajabu kuu ya kiroho ulimwenguni.

Hii inatuongoza katika ajabu ya tano, ambayo tunaitaja kama, 'Azimio kuu ulimwenguni.' Wakati Yesu alipokuwa ulimwenguni, alitembelewa usiku na Rabi mkuu wa Wayahudi kwa jina Nikodemu (Yohana 3:1-21). Kwa melezo mengine, Yesu alimwambia huyu Rabi, '*Mimi nitakwenda juu ya msalaba kwa kuwa Mimi ndimi mwana wapekee wa Mungu, nami ndiye suluhisho la kipekee kwa shida ya dhambi nami ndiye mwokozi wa pekee wa Mungu. amwanimiye yeye ahukumiwi; asiyeamimi amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu ya hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.'*

Mungu tayari ameupatia ulimwengu agano au mkataba wa kuokoa maisha. Yesu ameweka sahihi yake katika mkataba huo kupitia damu Yake Mwenyewe, lakini kuna nafasi yako na yangu ambayo tunahitajika 'kuitia sahihi' kwa njia ya imani yetu. Jambo hili linafanya uamuzi wa kuamini kile Yesu alichosema kuhusu yeye mwenyewe kuwa ndio azimio kuu ulimwenguni - na mojawapo ya ajabu la ulimwengu. Kweli kwamba azimio tunaofanya linaweza kumaanisha tofauti kati ya uzima wa milele na hukumu linafanya hukumu hiyo ya ajabu kuwa mojawapo ya kiroho katika ulimwengu.

Je! Wewe unawezaji kufahamu wakati umefanya azimio ya milele? Katika Maandiko, neno la Kiyunani la 'kuamini' halikumaanisha makubaliano ya kiakili. Wala sio kupunga kichwa chako kama ishara ya mwitikio na kusema, 'Mimi naamini hicho.' Mtu mmoja alitoa mfano huu kwa njia ya kamba ndefu kutoka pande moja ya maporomoko makuu ya maji huko Marekani. Aliendesha baisikeli lake kutoka upande moja hadi mwingine na kurudi tena. Makutano

yaliyohudhuria maonyesho hayo walipiga makofi kwa kushangilia. Naye akawauliza, *'Ni wangapi miongoni mwenu ambao wanaweza kuamini kwamba mimi ninaweza kutenda hivi kwa mara nyingine na kwa kumbeba mtu mwingine pamoja nami juu ya baisikeli hii?'* Wachache kati yao wakainua mikono, naye akamchagua mmoja kati yao na kusema, 'shika usukani wa baisikeli hii!' Yule mmoja kati ya makutano akasema, 'La! Sio mimi!' huku mtu huyo akimjibu, *'Basi ni wazi kabisa kwamba wewe hauamini yawezekana.'*

Neno la Kiyunani la 'kuamini' hakika maanake ni 'Panda juu ya baisikeli.' Ikiwa wewe ungelikuwa mtu ambaye hajiwezi na nyumba yako ichomeke kwa moto, naye mtu aje katika chumba chako cha kulala na kukupatia msaada wa kukubeba nje, kwa hakika itakubidi kuwekelea uzito wote wa mwili wako juu ya yule mwokoaji na kuweka tumaini lako kwamba atakubeba kutoka ndani ya hiyo. Hii ni moja ya njia ambayo tafsiri moja ya Biblia inatafsiri neno 'kuamini' katika msitari ule wa kumi na sita katika sura ya tatu kwenye Injili ya Yohana: *'Ye yote yule ambaye huegemeza uzito wake wote juu ya Yesu hatapotea, bali ataupata uzima wa milele.'* Wewe unaamini kikamilifu wakati unapoweka wokovu wako katika ungamo la tangazo lake Yesu kwamba Yeye ndiye mwana wa pekee wa Mungu, suluhisho na mwokozi wa kweli.

Na Je! utafahamu ni kwa njia ipi hakika umeamini? Ajabu ya sita ni 'mwelekeo mkuu katika ulimwengu.' Katika vitabu vya Injili, tunasoma kwamba kila wakati mtu anaposema kwa Yesu kuwa, 'mimi ninaamini wewe.' Alinena maneno haya mawili kwao. Maneno haya ni: 'Nifuate Mimi.' Wakati waliposikia maneno hayo, wao walitambua kwamba kumfuata Yeye, iliwabidi kubadilisha maisha yao na kugeuka mbali na maisha yale waliyokuwa wakiishi. Wengi kati yao hawakutaka kutenda hivyo, na kwa sababu hiyo, hawakumfuata Yeye. Wao waligundua kwamba kwa hakika hawakumwamini.

Hata hivyo, kulikuwa na kikundi kidogo kilichojitolea kwake na kumwamini pamoja na kumfuata. Waligundua kwamba mwelekeo wa kumfuata Yesu ndio mkuu duniani. Yeye alithibitisha agano nao, agano iliyokuwa, *'nifuateni Mimi nami nitawafanya ninyi* **(Mathayo 4:19).'** Walipoazimia kujitolea na kumfuata Yeye, Aliwafanya kuwa kile alichotaka. Miaka sitini baadaye, mmoja wao aliweka wakfu kitabu cha mwisho katika Biblia kwake Yesu kwa maneno haya, *'Kwake Yeye aliyetupenda sisi, na kutufanya wafalme na makuhani. . .'* Kwake mtume Yohana, mwelekeo wa kumfuata Yesu ni ajabu ya kiroho katika ulimwengu.

Ajabu ya saba ya kiroho ni 'uweza mkuu duniani.' Sisi hatuwezi kufahamu jambo hili kwa ukamilifu, lakini Yesu alifundisha kwamba wakati tunapoazimia kumfuata, huwa tunapata ushuhuda wenye kubadilisha ambao ni kama kuzaliwa kwa mara nyingine. Kwa kupitia muijiza, Roho Wake Mtakatifu hufanya makao yake ndani ya mwili wako, nasi hupata ushuhuda wa uweza mkuu duniani. Uzao huu mpya, Kristo akiishi ndani mwetu, hutupatia uwezo tunaohitaji ili kumfuata Kristo.

Haya ndio baadhi ya mambo saba ya kuvutia ninayofahamu. Mtindo mkuu ulimwenguni, talaka kuu ulimwenguni, shaka kuu ulimwenguni, tangazo kuu ulimwenguni, azimio kuu ulimwenguni, mwelekeo mkuu ulimwenguni, na uweza mkuu ulimwenguni. Ninayataja kama, 'maajabu saba ya kiroho ulimwenguni.'

Unaweza kufanya uamuzi kuelekea katika mwelekeo wa kumfuata Yesu Kristo na kupokea kutoka kwa Kristo aliyefufuka uweza wa kuzaliwa kwa mara ya pili. Muijiza huu wa uzao mpya huanza wakati wa azimio la kuamini. Je! Ungependa kufanya azimio hilo wakati huu?

Kuamini maajabu haya saba ya kiroho ulimwenguni kutakupatia msingi ambao unaweza kufanya ndoa mbele za Mungu. Ni lazima uwe na ushuhuda wa neema ya wokovu na pendo la Kristo kwa ajili yako mwenyewe, kabla ya kuhusika na mwenzio katika ndoa na katika njia ya upendo inayolingana na Kristo jinsi nimekueleza hapo mwanzoni katika masomo haya. Bila msingi huu wa kiroho, ndoa yako haitakuwa jinsi Mungu alikusudia iwe.

Maombi na hamu yangu ni kwamba Mungu atakusaidia kutimiza kanuni hizi katika ndoa na jamii yako, kuanzia wokovu wako na uhusiano wa kiroho na wa kipekee kati yako na Mungu.